# Uelekeo

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

## Serikali yaishukia Yanga



Uk. 24

| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00042 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano Desemba 13 - 19, 2023 |



Uk.12

### Rais Samia anavyotoa majibu sahihi kwa wahafidhina



Uk. 19

### 'Israel haitakaa kwa muda mrefu Gaza'



Uk.2

### NIDA yawaita wakazi Dar kuchukua Vitambulisho

# 'Pikipiki za Samia ziboreshe kilimo'



Uk. 4

Rais Dk. Samia, anafanya uwekezaji mkubwa katika utekelezaji wa Ajenda 10/30 kilimo biashara kwa kuwanunulia maofisa ugani wote nchini pikipiki, vishikwambi, vipima afya ya udongo na lamination machine na kuanza utekelezaji wa kuwajengea nyumba katika vituo vyao vya kazi walipo wakulima.




## NEMC: Fukwe za bahari si salama



Uk. 7

Uk. 3



## Makonda achangia mil. 10/- Taasisi ya Prof. Jay



## Makala aifagilia ATCL

Uk. 3

Uk. 14 &15



## Sawa Nape, Serikali isifumbie macho wahuni mitandaoni

## EU yaimwagia Tanzania magari ya bilioni 1.9/-

Uk. 4

# NIDA yawaita wakazi Dar kuchukua Vitambulisho

**Na Mwandishi Wetu**



MAMLAKA ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), imesema ugawaji wa Vitambulisho vya Taifa kwa wakazi wa wilaya zote za Mkoa wa Dar es Salaam, ulitarajiwa kuanza jana na utadumu ndani ya siku 14.

Kwa msingi huo, NIDA imewataka wananchi wote waliosajiliwa na kupatiwa Namba za Utambulisho wa Taifa (NINs), kwenda katika ofisi za serikali za mitaa yao kuchukua vitambulisho vyao.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Kitengo cha Mawasiliano cha NIDA, kwa mwananchi atakayeshindwa kuchukua Kitambulisho chake cha Taifa ndani ya muda uliopangwa katika eneo lake, atalazimika kukifuata katika ofisi ya NIDA ya wilaya anayoishi.



## Uzoaji tope, ufunguaji barabara waendelea Katesh

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama, ameendelea na usimamizi wa uzoaji tope na ufunguaji wa barabara katika Mji wa Katesh Halmashauri ya Wilaya ya Hanang.

Mbali na kufungua barabara, Waziri Mhagama aliendelea kushiriki kupokea misaada mbalimbali kutoka kwa wananchi na wadau wenye mapenzi mema.

Aidha, mwitikio wa wananchi ni chanya katika tukio la kuhifadhi waathirika wa maporomoko ya mawe na matope kutoka mlima Hanang kwa kushrikiana na serikali.

Uratibu wa zoezi hilo unaenda sanjari na ugawaji wa vifaa vya msaada wa kibinadamu kwa waathirika wa maafa hayo.

Hatua hiyo inaenda sambamba na hali ya urejeshaji hali katika Mji wa Katesh, Halmashauri ya Wilaya ya Hanang mkoani Manyara, huku shughuli ya uondoaji wa tope katika barabara na mitaa ya Mji wa Katesh ikiendelea.

## Dawati la Jinsia latakiwa kutoa elimu zaidi

**Na Abel Paul, Jeshi Polisi, Dodoma**

KAMISHNA wa Utawala na Menejimenti ya Rasilimali Watu, CP Suzan Kaganda, amewataka watendaji wa Dawati la Jinsia na Watoto kote nchini, kutoa elimu zaidi ili kumaliza vitendo vya ukatili katika jamii.

Hata hivyo, CP Kaganda amewapongeza watendaji wa uwezo mzuri watendaji wa Dawati la Jinsia na Watoto.

Kwa upande wake, Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto, Naibu Kamishna wa Polisi DCP, Maria Nzuki, alisema kutokana na kazi nzuri ya kutoa elimu kwenye nyumba za ibada iliyofanyika Jumapili katika makanisa mbalimbali jijini Dodoma, tayari makanisa zaidi ya 20 yameomba Watendaji wa Dawati hilo



dawati hilo kwa kufuatilia kesi za ukatili kwa karibu na wahusika kufikishwa mahakamani.

Aliyasema hayo jana wakati wa mkutano na Watendaji wa Dawati la Jinsia na Watoto kutoka Mikoa ya Tanzania Bara na Zanzibar unaoendelea jijini Dodoma.

CP Kaganda aliongezea kuwa Jeshi la Polisi nchini litaendelea kuwatumia watalaamu wa ndani na nje ya nchi ili kuwajengea kuwapatia elimu ili kuwaongezea maarifa ya namna bora ya kutatua changamoto za ukatili wa kijinsia.

Pia alibainisha kuwa Madawati ya Jinsia na Watoto ambayo yapo chini ya Jeshi la Polisi, yameendelea kuwa kimbilio katika kubaini na kuzuia vitendo vya ukatili wa kijinsia hapa nchini ambapo wananchi wengi wamezidi kuwa na uelewa mzuri zaidi juu ya vitendo vya ukatili.

# Mkandarasi aagizwa kukamilisha mradi wa maji

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, amewataka wakandarasi wa mradi wa maji wa Mugango hadi Kiabakari mpaka Butiama, waongeze juhudi ili wakamilishe kwa wakati kuwezesha zaidi ya wananchi 233,000 wanufaike na huduma ya maji safi na salama.

Mhandisi Mahundi alitoa rai hiyo juzi wilayani Butiama mkoani Mara, wakati wa ziara yake ya kukagua utekelezaji wa ujenzi wa mradi wa maji wa Mugango hadi Kiabakari mpaka Butiama na mradi wa maji wa Kijiji cha Kyankoma hadi Kiagata.

Katika ziara hiyo, Mhandisi Mahundi aliwasisitiza wakandarasi hao kukamilisha utekelezaji wa miradi hiyo ili wananchi wapate huduma ya maji safi na salama.

"Mwishoni mwa Desemba, mwaka huu, mradi huu uwe umekamilika kulingana na mkataba wa nyongeza. Pia, namuagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Mugango/Kiabakari, kusimamia utekelezaji wa mradi huu," alisisitiza Mhandisi Mahundi Kadhalika, Mhandisi Mahundi alizindua mradi wa maji wa Kijiji cha Kyankoma hadi Kiagata unaotekelezwa na fedha za P for R kwa gharama ya Sh. million 609.2 na kwamba kukamilika kwake, utanufaisha zaidi ya wakazi 5,200.

Kwa upande wake, Mbunge wa Jimbo la Butiama, Jumanne Sagini ambaye pia ni Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, aliishukuru serikali kwa utekelezaji wa ujenzi wa mradi wa maji wa Mugango – Kiabakari – Butiama.

Alisema mradi huo unatumia chanzo cha maji cha uhakika cha Ziwa Victoria na kwamba kukamilika kwa mradi huo kutapunguza kero ya ukosefu wa maji katika eneo hilo.

## Taasisi ya Uhasibu Tanzania yatua Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu, Zanzibar**

WAZIRI wa Fedha na Mipango wa Zanzibar, Dk. Saada Mkuya Salum, amesema ujio wa Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) Zanzibar, utasaidia kuinua kiwango cha elimu ya uhasibu visiwani humu.

Aliyasema hayo alipokuwa akizindua kampasi ya saba ya chuo hicho tawi la Mjini Unguja Visiwani Zanzibar.

Dk. Mkunya alisema, mahitaji ya elimu ni mengi kwa sasa, hivyo kuanzishwa kwa tawi hilo kutasaidia kukidhi mahitaji.

"Hatua hii ni ya kupongezwa na kwamba itafikia matarajio ya Serikali katika kuongeza wataalamu katika sekta muhimu nchini, ufunguzi wa tawi hili unakuja wakati sahihi hasa ukizingatia kuna watumishi wengi wenye vikwazo vya kufuata masomo nje ya Zanzibar," alisema



Dk. Mkuya.

Aidha alisema chuo hicho kitarahisisha watumishi wenye nia ya kujiendeleza pamoja na kutumia muda wa baada ya kazi kuendelea na masomo kupitia taasisi hiyo.

Dk. Mkuya alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itaendelea kushirikiana na taasisi hiyo ili kuona wanatoa wasomi wenye viwango vizuri huku akiuomba uongozi wa TIA kufungua tawi lingine kisiwani Pemba ili wananchi walio wengi wanufaike kada hiyo.

Naye, Ofisa Mtendaji Mkuu wa TIA, Profesa William Ballargyo, aliipongeza serikali kwa ushirikiano uliokuwepo kati yao na kuahidi kuweka vipaumbele muhimu katika udahili ili kuona wenye sifa wanapata fursa ya kujiunga na kampasi hiyo.

Alisema Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania inatenga Sh, bilioni tatu kupitia Wizara ya Fedha kwa ajili ya hatua ya awali za ujenzi.

Akizungumzia mpango wa baadaye wa chuo hicho, Meneja Mmiliki wa taasisi hiyo, Mhandisi Masuhuko Nkuba, alisema wanatarajia kujenga majengo yao ya kudumu katika Kijiji cha Nganani Makunduchi na kwamba kwa hatua za awali wataanza na jengo litakalochukua wanafunzi 1,000.

TIA kwa sasa inaedesha masomo hayo katika jengo la Thabit Kombo kwa kutoa masomo mbalimbali yakiwamo Uhasibu, Ugavi na Teknolojia ya Habari na Manunuzi.

# Waziri Mbarawa ashuhudia majaribio SGR



Na Mwandishi Wetu

WAZIRI wa Uchukuzi Profesa Makame Mbarawa, amefanya ziara fupi ya kuona majaribio ya kichwa cha treni ya umeme cha reli ya kiwango cha kimataifa (SGR) kilichopo kwenye Stesheni ya Pugu jijini Dar es Salaam.

Profesa Mbarawa alifanya ziara hiyo juzi akiwa na lengo la kuona uwezo wa kufanya kazi kichwa hicho cha SGR ambacho kwa sasa kipo kwenye majaribio mbalimbali.

"Majaribio ya kwanza yanafanyika ikiwamo mifumo ya breki, mifumo ya breki za umeme na upepo na mwendokasi wa kilomita 160, nimeridhika kwamba kichwa hiki kipo vizuri na kina uwezo mkubwa," alisema Profesa Mbarawa.

Aidha, alisema kichwa hicho ni moja kati ya vichwa 17 ambavyo Serikali imenunua kutoka nchini Korea Kusini vyenye thamani ya Sh. bilioni 254 ambapo vichwa vingine vitatu vinatarajiwa kufika mwishoni mwa mwezi huu.

"Baada ya majaribio haya, awamu ya pili inayofuata ni kukifunga kichwa hiki na mabehewa kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro," alifafanua Profesa Mbarawa.

Hata hivyo, Waziri Profesa Mbarawa aliwasihi wananchi kuendelea kuwa na subira na punde majaribio yatakapokamilika na kujiridhisha kuanza kwa safari za abiria na mizigo, wananchi watafaidi matunda ya SGR.

Alisema SGR itatoa fursa na kurahisisha maisha ya Watanzania kwa kutumia mwendokasi wa kilomita 160 kwa saa ambapo itatumia mwendo wa saa moja na nusu kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro, saa tatu Dar es Salaam hadi Dodoma na saa saba kutoka Dar es Salam hadi Mwanza.

# Makonda achangia mil. 10/- Taasisi ya Prof. Jay



Na Mwandishi Wetu

TANGU kuanzishwa kwa kampeni ya kuchangia Taasisi ya Profesa Jay Foundation kwa ajili ya wagonjwa wa figo, vigogo mbalimbali wakiongozwa na Mwenyekiti Taifa wa Chama Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Dk. S amia Suluhu Hassan, Katibu wa NEC, Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM Taifa, Paul Makonda, ameunga mkono kampeni hiyo.

Makonda ameunga mkono juhudi za kampeni hiyo kwa kuchangia Sh. milioni 10 kufanikisha malengo ya taasisi hiyo.



# RC Makala aifagilia ATCL




Na Mwandishi Wetu

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla, amesema Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL), ina uwezo mkubwa wa kubeba bidhaa mbalimbali kwa kutumia ndege yake mpya ya kisasa ya mizigo aina ya Boeing 767-300F.

Akizungumza wakati wa kikao cha pamoja cha wadau wa soko la bidhaa za samaki kutoka mkoani Mwanza kilichofanyika ATCL Makao Makuu jijini Dar es Salaam, Makalla alisema kuwepo kwa ndege hiyo kunarahisisha usafirishaji wa bidhaa za Tanzania.

"Ndege hii itarahisisha usafirishaji wa bidhaa zetu hapa nchini ikiwamo minofu ya samaki itakayosafirishwa moja kwa moja kutoka Kanda ya Ziwa kwenda kwenye masoko mbalimbali duniani," alisema.

Alisema ndege hiyo inawawezesha wafanyabiashara wa minofu ya samaki kupunguza gharama za uzalishaji na kuongeza thamani ya minofu kwa kutumia muda mfupi kufika kwenye soko la walaji.

Aidha, Makalla aliwahakikishia wafanyabiashara hao kuwa wataendelea kushirikisha wadau na wataalam mbalimbali katika kushughulikia changamoto zilizopo ikiwa ni pamoja na kuboresha miundombinu ya Uwanja wa Ndege wa Mwanza hususan jengo la kuhifadhia bidhaa, uwepo wa kituo kimoja cha utoaji wa huduma za mamlaka zote za uthibiti kupitia tozo na taratibu ili kupunguza gharama zisizo za lazima na kuhakikisha bidhaa hizo zinasafirishwa kupitia Uwanja wa Ndege wa Mwanza.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa ATCL, Ladislaus Matindi, alisema Air Tanzania pamoja na kufanya biashara, inahusika pia na uwezeshaji wa sekta nyingine kwa kutoa huduma zinazohitajika ikiwamo kulinda thamani ya bidhaa za Watanzania kwa kuzifikisha kwenye soko la dunia zikiwa shindani.

Matindi aliongeza uwepo wa ndege ya mizigo yenye uwezo wa kubeba mizigo yenye upana mkubwa na uzito wa zaidi tani 50 kwa mara moja, ni fursa kwa Watanzania kukuza biashara zao duniani.

# 'Pikipiki za Samia ziboreshe kilimo'




**Na Mwandishi Wetu, Tanga**

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, amesema katika jitihada za utekelezaji wa ajenda 10/30 ni muhimu uwekezaji mkubwa uliofanywa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, katika kilimo ikiwemo kumwaga pikipiki nchi nzima kwa maofisa ugani, utoe matunda yaliyokusudiwa.

Itakumbukwa kwamba Rais Dk. Samia aliwanunulia maofisa ugani wote nchini pikipiki, vishikwambi, vipima afya ya udongo na kuanza utekelezaji wa kuwajengea nyumba katika vituo vyao vya kazi walipo wakulima.

Ni kwa muktadha huo, Waziri Bashe amewataka wakurugenzi wa halmashauri zote nchini kuhakikisha kwamba maofisa ugani wanapatikana katika vituo vyao vya kazi kama ilivyo kwa walimu ili kwenda sambamba na juhudi za Rais Dk. Samia katika kukuza kilimo.

Ajenda 10/30 inalenga kuona sekta ya kilimo (sekta ndogo ya mazao) ikikua kwa asilimia 10 ifikapo 2030 na hivyo kuchangia katika kupunguza umaskini nchini.

Waziri Bashe jana ambaye alikuwa katika siku yake ya kwanza ya ziara ya siku tatu mkoani Tanga alikumbusha: "Rais Dk. Samia, anafanya uwekezaji mkubwa katika utekelezaji wa Ajenda 10/30 kilimo biashara kwa kuwanunulia maofisa ugani wote nchini pikipiki, vishikwambi, vipima afya ya udongo na lamination machine na kuanza utekelezaji wa kuwajengea nyumba katika vituo vyao vya kazi walipo wakulima."

Alisisitiza kuwa maofisa ugani wote wajiwekee mfumo wa kutoa taarifa ya utekelezaji wao wa majukumu ikiwamo taarifa za wakulima waliowatembelea na changamoto walizozitatua.

Alisema Wizara ya Kilimo haitamvumilia ofisa ugani yeyote asiyeendana na kasi ya utekelezaji wa malengo mapana ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia.

## EU yaimwagia Tanzania magari ya bilioni 1.9/- miradi ya umeme

**Na Mwandishi Wetu**

UMOJA wa Ulaya (EU) umeipatia Serikali ya Tanzania magari 21 kati ya 29 yenye thamani ya Sh. bilioni 1.9 kusaidia kurahisisha utekelezaji wa miradi ya Wakala wa Nishati Vijijini (REA).

Akipokea magari hayo jijini Dar es Salaam jana, Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga, aliishukuru EU kwa kuendelea kuisadia Serikali ya Tanzania katika miradi mbalimbali ikiwemo huu wa usambazaji wa nishati vijijini.

Judith alisema hii si mara ya kwanza EU kuisaidia Serikali ya Tanzania kwani wamekuwa wakisaidia katika miradi mbalimbali ikiwemo Kituo cha Kupoza Umeme Ifakara (20MVA wa kuzalisha megawati 16).

Hata hivyo, aliitaka REA kuyatumia vizuri magari hayo ili kuhakikisha dhamira ya kuwaletea wananchi maendeleo inafikiwa.

Kwa upande wake, Mwakilishi wa Balozi wa EU nchini, Cedric Merej, alisema ni fahari kwao kushiriki katika utekelezaji wa mradi huo utakaoleta tija kwa wananchi wa vijijini.

Merej alisema wanaamini kwamba msaada huo utagusa asilimia 30 ya wananchi wa vijijini, jambo ambalo ni matokeo chanya na makubwa tunayoyatarajia

Naye Mkurugenzi Mkuu wa REA, Hassan Saidy, aliahidi kuyatunza vizuri na kusimamia matumizi sahihi ya magari hayo ikiwa ni moja ya mradi kati ya miradi kadhaa iliyokwisha kutekelezwa.

"Wamechangia utekelezaji wa miradi mikubwa minne. Kuna mradi wa kupeleka umeme vijijini, awamu ya tatu, mzunguko wa kwanza. Pia wamechangia mradi wa ujazilizi awamu ya pili A," alisema.

Aidha, alisema EU pia kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania, wanatekeleza miradi ya umeme inayoendelea maeneo ya Ifakara, Ulanga na Mvomero, pia mikakati ya serikali ni kuhakikisha taifa linahamia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia.

# Katekista ahukumiwa kunyongwa hadi kufa

**Na Mwandishi Wetu, Njombe**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Iringa iliyofanya kikao chake mkoani Njombe, imemhukumu kunyongwa hadi kufa, Kateksta Daniel Philipo Mwelango (42), mkazi wa Makambako baada ya kukutwa na hatia ya mauaji ya kukusudia ya Katibu wa Walei Kanisa Katoliki Kaigango cha Parokia ya Makambako, Nickson Elias Myamba (43).

Akisoma hukumu hiyo, Jaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Iringa, Said Kalunde, alisema mshtakiwa alitekeleza mauaji hayo Agosti 2, mwaka jana mtaa wa Bwawani katika duka la Kanisa Katoliki Kigango cha Makambako.

Jaji Kalunde alisema siku ya tukio, mshitakiwa ali andaa panga, chuma na mifuko minne ya kinganjaa kwa ajili ya kuzuia damu isisambe na mifuko miwili mingine ya kuhifadhia mwili wa marehemu.

Baada ya hapo, mshtakiwa alimpiga na chuma kwenye kisogo na alipoanguka chini, alimkata vipande viwili na kuviweka katika mifuko ya kinganjaa ili iwe rahisi kubeba mwili huo na kwenda kuutupa mbali.

Aidha, Jaji alibainisha kuwa licha ya mshtakiwa kukiri kufanya kosa hilo kuwa hakukusudia, Mahakama kupitia upande wa mashitaka, imejiridhisha pasi na shaka juu ya ushahidi uliotolewa mahakamani hapo na hivyo kumkuta mshtakiwa na hatia ya mauaji.

Jaji Kalunde alisema kosa lililofanywa na mshtakiwa huyo ni kinyume cha kifungu cha sheria namba 196 na 197 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 marejeo ya mwaka 2022.

Upande wa utetezi kesi hiyo ilisimamiwa na Wakili Alex Mgani na kwa upande wa serikali ilisimamiwa na Wakili Magdalena Hyasint Whero ambaye aliiomba mahakama itoe adhabu kali dhidi mshtakiwa ili liwe fundisho kwa wengine kwani kitendo alichokifanya ni cha kikatili na hakikubaliki katika jamii.

**Baada ya hapo, mshtakiwa alimpiga na chuma kwenye kisogo na alipoanguka chini, alimkata vipande viwili na kuviweka**

# Samia atoa darasa la Kiswahili

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, ametoa darasa kwa Watanzania kuhusu matumizi ya Kiswahili fasaha ya maneno 'wahanga' na waathirika.

Rais Dk. Samia alieleza kwamba `wahanga' ni watu wanaojitolea kupigania taifa lao na 'waathirika' ni watu waliopatwa na maafa kama ya moto au mafuriko yaliyotokea Katesh Wilaya ya Hanang mkoani Manyara.

Alitoa somo hilo juzi alipompokea Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, aliyerejea nchini akitokea kutekeleza majukumu aliyomtuma.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan

"Juzi (wiki iliyopita), nilikuwa naongea na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, nikamsikia kila anapoongea anasema wahanga wamefikia…wahanga… nikamwambia Waziri Mkuu wahanga ni wale wanaokwenda kwenye tukio kwa ajili ya nchi yao, wakifa kule wale ni wahanga," alisema na kuongeza:

"Lakini hawa wa Hanang, ni waathirika, tukio limetokea limewaathiri wale ni waathirika, alikufa kwa ajali ya gari, wahanga hapana, wale waliokufa Msumbiji kupigania uhuru, ni wahanga, vita vya Majimaji, wale ni wahanga."

# Mhudumu wa Afya MNH abuni kitanda cha kumsaidia mgonjwa

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Profesa Mohamed Janabi, amezindua kitanda kinachotumika kumshusha na kumpakia mgonjwa kwenye gari la wagonjwa.

Kitanda hicho kimetengenezwa na Mhudumu wa Afya, Erasto Francisco, kwa lengo la kusaidia kutatua changamoto wanazokutana nazo wanapotoa huduma hiyo.




Akizungumza wakati wa kupokea kitanda hicho, Profesa Janabi alisema kazi ya kumpakia na kumshusha mgonjwa kwenye gari, ina changamoto nyingi kwa kuwa wagonjwa wengine wanakuwa na uzito mkubwa na endapo mtumishi atafanya kazi hiyo kwa muda mrefu inaweza kumsababishia kupata matatizo ya mgongo.

Profesa Janabi alimpongeza mtumishi huyo wa afya kwa ubunifu huo.

# Miaka 30 jela kwa ubakaji

**Na Mwandishi Wetu, Njombe**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Wanging'ombe mkoani Njombe, imemhukumu miaka 30 jela Ezekiel Ngilangwa (22), mkazi wa Imalinyi kwa kosa la ubakaji.

Ngilangwa alitenda kosa hilo Oktoba 30, mwaka huu katika Kijiji cha Imalinyi ambapo alimbaka mwanafunzi wa Shule ya Msingi Imalinyi, Wanging'ombe.

Hukumu hiyo ilitolewa mbele ya Hakimu James Emmanuel Muhoni.

# Misaada yazidi kumiminika Hanang

**Na Mwandishi Wetu, Katesh**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kwa kushirikiana na Umoja wa Kampuni za Bima Tanzania (ATI), wametoa msaada wa vitu mbalimbali vikiwamo vyakula na vifaa kwa waathirika wa maafa yaliyotokea Desemba 2, mwaka huu katika Wilaya ya Hanang mkoani Manyara.

Akikabidhi vifaa hivyo, Kamishna wa Bima, Dk. Baghayo Saqware, alisema kwa pamoja walivyoguswa na tukio hilo, alizialika Kampuni za Bima ili washiriki kwa umoja wao kuchangia walichonacho kuwasaidia waathirika hao.

Alivitaja vitu walivyokabidhi kuwa ni, vyakula, vyombo, nguo, sabuni na mabegi ya kuhifadhia nguo.

Dk. Saqware alisema mchele ni kilo 2,400, maharage kilo 1,200, sukari kilo 100, ngano kilo 500, mafuta ya kupikia lita 1,080, maziwa ya Kopo 48, sahani 209, vikombe 202, mabegi ya kuhifadhia nguo matano, unga wa lishe kilo 22, chupa za chai 72, sabuni za maji dumu 12, sabuni za miche 400 na sabuni za kunawia mikono chupa 72 pakiti 1,200 za chumvi.

Akipokea msaada huo, Mkuu wa Wilaya ya Hanang, Janeth Mayanja, alisema msaada uliotolewa na sekta ya bima unagusa waathirika kwa kiasi kikubwa hasa kwa kuzingatia mahitaji ya watoto wadogo kwa kuwapatia maziwa na unga wa lishe.

Alisema kwa kuhamasisha taasisi nyingine na watu binafsi kuiga mfano wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima na Kampuni za Bima kuja kujitolea kwa chochote watakachojaliwa.



Wa kwanza kushoto ni Dk. Baghayo Saqware, Kamishna wa Bima (TIRA) anayefuata ni Mtendaji Mkuu wa Umoja wa Kampuni za Bima Tanzania, Elia Lajiba, katikati ni, Mkuu wa Wilaya ya Hanang, Janeth Hayanja na wa kwanza kulia ni Mwakilishi wa Kampuni za Bima, Gerald Awendo. Picha: Mpigapicha Wetu.

# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi


## HII NI KERO

### Makondakta oneshani uungwana



Hivi karibuni, serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) ilipandisha nauli za mabasi ikiwemo daladala. Katika jiji la Dar es Salaam, nina hakika hadi leo kuna watu hawajajua kama nauli zimepanda na wapo makondakta ambao hawasemi kabla ya kupakia abiria kuhusu kupanda kwa nauli.

Jana nimeona kondakta akimmwagia matusi abiria aliyetoa Sh 500 kwa sababu hakujua kama nauli imepanda. Ni vyema makondakta wawe waungwaa na kuwasaidia abiria ambao hawajajua kwamba nauli zimepanda. Ni suala la muda mfupi, kila mtu atajua nauli imepanda.




## MAONI YA MHARIRI

# Maofisa ugani wasimamiwe ipasavyo

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, amekuwa akifanya uwekezaji mkubwa katika kilimo ili kutekeleza Ajenda ya 10/30 inayolenga kuona sekta ya kilimo (sekta ndogo ya mazao), inakua kwa asilimia 10 ifikapo mwaka 2030.

Imani iliyopo ni kwamba ukuaji huo ukifikiwa, kilimo ambacho kinaajiri zaidi ya asilimia 60 ya Watanzania, kitachangia sana katika kupunguza umaskini nchini.

Moja ya uwekezaji uliofanywa na Rais Dk. Samia ni kuwanunulia maofisa ugani wote nchini pikipiki, vishikwambi, vipima afya ya udongo na mashine za lamination.

Sambamba na hilo, serikali ilianza utekelezaji wa kuwajengea maofisa ugani hao nyumba katika vituo vyao vya kazi kwa maana ya mahali walipo wakulima.

Rais pia aliamua kuwamilikisha pikipiki hizo baada ya kuzitumia kwa miaka miwili, hususani wale ambao utendaji wao utaridhisha. Hapo watake nini tena!

Tangu maofisa ugani hao wakabidhiwe vitendea kazi hivyo ili wawasaidie wakulima kuondokana na changamoto katika kuelekea kwenye kilimo bora kinachowapa mazao mengi katika eneo dogo, sasa ni takribani mwaka na ushee. Je, mafanikio yakoje?

Katika kuhakikisha maofisa ugani ambao kimsingi wako chini ya halmashauri mbalimbali, jana Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, aliwataka wakurugenzi wa halmashauri zote nchini kuhakikisha maofisa ugani wanapatikana katika vituo vyao vya kazi muda wote kama ilivyo kwa walimu.

Waziri Bashe alitoa angalizo na msisitizo huo akiwa katika siku yake ya kwanza ya ziara ya siku tatu mkoani Tanga.

Tunampongeza Waziri kwa kutoa maelekezo hayo kwa wakurugenzi wote tukiamini kwamba watayafanyia kazi ipasavyo.

Kama alivyosema Waziri, ni vyema wakurugenzi wakahakikisha pia kwamba maofisa ugani wote wanajiwekea mfumo wa kutoa taarifa ya utekelezaji wao wa majukumu ikiwamo taarifa za wakulima waliowatembelea, changamoto walizokutana nazo, walizozitatua na zilizowashinda.

Ni vyema Wizara ya Kilimo na halmashauri visimvumilie kabisa ofisa ugani asiyetekeleza majukumu yake na huyo hafai hata kumilikishwa pikipiki.

Tunaamini kama kila ofisa ugani akitimiza wajibu wake kwa kwenda na kasi ya utekelezaji wa malengo mapana ya Serikali ya Awamu ya Sita, ajenda 10/30 inaweza kufikiwa hata kabla ya mwaka 2030.

## Wasiliana nasi


| | |
|---|---|
| **Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000 | **S. L. P:** 15110, Dar es Salaam |
| **Mhariri wa Habari:** +255768411003 | **Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro |
| **Mhariri Michezo:** +255787559090 | **Jengo la:** Aura Mall |
| **Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825 | **Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532 |
| | **Email:** uelekeohabari@gmail.com |





Na Hamisi Kibari

JICHO LANGU

Simu: 0758143457


# Ni wachache ambao kwao mteja ni mfalme

PROFESA Joseph Mbele, Mtanzania aliyekuwa akiishi Marekani aliwahi kuandika makala kuhusu Watanzania wasivyo makini linapokuja suala la huduma kwa wateja. Sina hakika kama bado Mbele anaishi Marekani au alisharudi nyumbani.

Kutokana na makala ile ya siku nyingi kidogo, niligundua kwa nini nilipokwenda Arusha nilona watumishi wengi katika hoteli za kitalii ni Wakenya. Hii ikanionesha kwamba linapokuja suala la huduma kwa wateja hawa wenzetu wanatuzidi!

Juzi nilikuwa kwenye mgahawa mmoja, nikakumbuka andiko la Profesa kwa jinsi huduma zilivyokuwa hovyo.

Profesa huyo alisema wapende wasipende, wafanyabiashara na watoa huduma mbalimbali wanajikuta katika mazingira ya mashindano ambayo yanaongezeka kwa kasi na yanazidi kuwa magumu. Katika hali hii akasema ni muhimu kwa kila mhusika kujua siri za mafanikio.

"Siri moja wapo ni ubora wa huduma. Kuna usemi kuwa mteja ni mfalme. Nimeona sehemu mbalimbali duniani ambapo dhana hii inazingatiwa sana. Wako watu wanaofahamu vyema umuhimu wa mteja. Wawe ni wafanyabiashara au watoa huduma, wanaonesha kumjali sana mteja. Hata kama mteja ni msumbufu wafanyabiashara na watoa huduma hao wako tayari kumsikiliza, kumvumilia na kumsaidia hadi aridhike," aliandika profesa huyo.

> **Siri moja wapo ni ubora wa huduma. Kuna usemi kuwa mteja ni mfalme. Nimeona sehemu mbalimbali duniani ambapo dhana hii inazingatiwa sana. Wako watu wanaofahamu vyema umuhimu wa mteja.**

Alitoa mfano kwamba nchini Marekani, mteja anaponunua kitu, anapewa risiti, na kama hataridhika na kitu alichonunua, ana uhuru wa kukirudisha na kurudishiwa pesa zake, au kubadilisha alichonunua akapata kingine, bora alete tu ile risiti.

"Hali hii si ya kawaida Tanzania, ambako risiti mara nyingi huwa imeandikwa "bidhaa ikishauzwa haiwezi kurudishwa dukani". Hata kwenye vyombo vya usafiri Tanzania, hali hii ni ya kawaida. Nimeona mara kwa mara tiketi za kusafiria zimeandikwa ujumbe kwamba tikiti ikishakatwa, haiwezi kurudishwa," alisema na kuhoji kwamba haoni sababu ya hali hiyo.

Akazidi kuaandika: "Nchini Marekani, nimeona kuwa wahudumu wanawaheshimu wateja. Wanafanya kila juhudi kumsaidia mteja. Kama mhudumu analegea katika kutoa huduma, labda kwa sababu ya kutoelewa, au kazidiwa na shughuli, mkuu wake wa kazi, hata meneja, yuko tayari kuja kutoa hiyo huduma. Si ajabu nchini Marekani kumwona meneja akitoa huduma ambayo kwa kawaida inatolewa na mfanyakazi wa chini yake. Tanzania nimeona mambo tofauti. Meneja wa hoteli, kwa mfano, hawezi kuchukua kitambaa na kusafisha meza ya mteja. Atamtafuta mhudumu wa hoteli aje asafishe. Meneja anajiona mtu bora kuliko wahudumu. Ni kawaida kumwona meneja amekaa kwenye meza na watu anaowajua yeye, na kazi yake ni kunywa pombe na kuongea nao na kuagiza!

Alisema alipokuwa kwenye baa na hoteli za Tanzania, aliwahi kuwaeleza mameneja ikiwemo malalamiko na ushauri kuhusu huduma, lakini mara kadhaa aligundua mameneja wameshalewa, na hawana uwezo wa kumsikiliza na kuzingatia aliyokuwa anasema.

"Naamini kuwa, ili tuweze kufanikiwa katika dunia ya ushindani, tabia hizi lazima tuzibadili," aliandika.

Nadhani kila mtoa huduma ni vyema azingatie angalizo hilo.

# NEMC: Fukwe za bahari si salama



Na Mwandishi Wetu

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limewataka wananchi kujiepusha kwenye maeneo ya fukwe za bahari, mito na maziwa kuepuka madhara yanayoweza kutokea kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha.

Tahadhari hiyo ilitolewa na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa baraza hilo, Menan Jangu, wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam juzi.

Alisema wananchi wanaoishi kando ya milima, wanapaswa kuchukua tahadhari kubwa kwani kuna uwezekano wa kutokea maporomoko ya udongo na kusababisha athari kwa maisha ya watu.

Aliwataka madereva wa vyombo vya moto, kuchukua tahadhari kubwa wakati wa safari kwa kuzingatia kuwa maeneo ya barabara yanaweza yakawa siyo salama.

Jangu aliwataka wamiliki wa maeneo ya uchimbaji na uchenjuaji wa madini kwenye mabwawa ya majitaka yenye tope sumu na maeneo ya kutunzia miamba ya sumu, kuhakikisha maeneo hayo hayaleti madhara kwa jamii.

Jangu alisema kwa kipindi cha miezi miwili, maeneo mbalimbali yamekumbwa na mvua ambazo zimeleta athari kubwa ikiwa ni pamoja na maafa yaliyojitokeza katika maeneo ya Katesh Wilaya ya Hanang mkoani Manyara.

Aidha, alisema taarifa kutoka katika Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), zinaonesha kuwa mvua za viwango tofauti zitaendelea katika maeneo mbalimbali nchini na kwamba zimekuwa kubwa na kuendelea kusababisha madhara kadhaa wa kadhaa.

Alisema mvua hizo zimesababisha mafuriko kwenye maeneo mbalimbali, hali iliyosababisha madhara kama vile makazi kuharibiwa na wananchi kukosa maeneo ya kujisitiri na wengine kupoteza maisha na baadhi kujeruhiwa.

"Miundombinu ya maji na barabara kwenye baadhi ya maeneo imeathirika na kupelekea huduma za usafiri kukwama, usalama wa maji kuathiriwa kutokana na mwingiliano wa maji yasiyo salama yanayotokana na mafuriko na maji ya matumizi ya nyumbani, hivyo kusababisha magonjwa ya kuambukiza ikiwa ni pamoja na magonjwa ya mlipuko," alisema.

Alisema eneo lingine la kuzingatiwa ni miundombinu ya kuhifadhi majitaka na topesumu kwenye migodi na kwamba mvua zinazoendelea zimesababisha miundombinu husika kujaa na mingine kuvujisha maji yenye sumu na kuathiri mazingira na hata mifugo kufa kwa baadhi ya maeneo.

## Kituo cha Afya Mtae chapatiwa vifaa tiba vya Sh. milioni 114

Na Mwandishi Wetu, Tanga

KITUO cha Afya Mtae Wilaya ya Lushoto mkoani Tanga, kimepatiwa vifaa tiba vikiwamo vya upasuaji kwa wajawazito wakati wa kujifungua vyenye thamani ya Sh. milioni 114 kwa lengo la kupunguza vifo vya wajawazito.

Kufuatoia hatua hiyo ya serikali, wakazi wa wilaya hiyo, wamemshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kuwapatia vifaa tiba hivyo.

Akikabidhi vifaa hivyo, Ofisa Huduma kwa Wateja wa Bohari Kuu ya Dawa (MSD) Kanda ya Tanga, Mary Isango, alisema wajawazito walikuwa wanalazimika kutembea umbali usiopungua kilomita 65 kufuata huduma katika Hospitali ya Wilaya, lakini sasa wataondokana na adha hiyo baada ya kituo hicho kupokea vifaa vya huduma za dharura hususan za upasuaji kwa wajawazito.

Kadhalika, Mganga Mfawidhi wa kituo hicho, Shafii Makamba, aliishukuru Serikali inayoongozwa na Rais Dk. Samia kwa kufanya maboresho makubwa kuipandisha hadhi zahanati ya Kijiji cha Mtae kuwa Kituo cha Afya ili wananchi wapate huduma bora na karibu na hivyo kuokoa maisha ya wajawazito.




## Mawasiliano Kilosa - Dumila yakatika

Na Mwandishi Wetu, Morogoro

MAWASILIANO ya barabara ya Dumila-Kilosa Mjini, yamekatika baada ya daraja la muda la Ilonga Msalabani na Mazinyungu, kusombwa na maji kufuatia mvua zinazoendela kunyesha mkoani Morogoro.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, jana alitembelea maeneo mbalimbali yaliyoathiriwa na mafuriko hayo na kuagiza Wakala wa Barabara nchini (Tanroads) kurejesha mawasiliano ya barabara zilizofungiwa kwa haraka ili shughuli za kiuchumi ziendelee.

Mvua hizo pia zilisababisha madaraja manne ya Mto Mazinyungu, Mkondoa, Ilonga na Uhindini, kuharibika na kufungwa kutumika.

Menejea Tanroads Mkoa wa Morogoro, Mhandisi Lazack Kyamba, alisema tayari wameshafanya tathmini ya athari iliyopo na watarejesha mawasiliano ya barabara ya Dumila - Kilosa pamoja na Mikumi -Kilosa ndani ya siku mbili.

## Polisi yahadharisha mvua zinazoendelea



Na Mwandishi Wetu

JESHI la Polisi nchini, limewataka wananchi kuchukua tahadhari wakati wa kuvuka mito, madaraja na makorongo yaliyojaa maji ya mvua.

Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, David Misime, alisema mvua zinazoendelea kunyesha hazina urafiki na yeyote.

Kwa mujibu wa Kamanda Misime, wamepokea taarifa mbalimbali za watu wazima na watoto, kufa maji wakati wakijaribu kuvuka mito na barabara zilizojaa maji na wengine wakiogelea kwenye mito, mashimo na madimbwi.

Aidha, aliwataka wazazi kuwaonya na kutowaruhusu watoto wao kwenda kucheza au kuogelea kwenye mito huku akiwasisitiza watu waliochimba mashimo na kuyaacha wazi, wayafukie ili yasihatarishe maisha ya binadamu.



Na Mwalimu Paul Masatu
Simu: +255 766 775 255

# Ondoa tabia kikwazo, jenga tabia wezeshi

LEO naorodhesha baadhi ya tabia ambazo ni kikwazo kwenye mafanikio yako. Kama unazo tabia hizi, hakikisha unaziacha kabla ya kuuanza mwaka mpya wa 2024

**1. Huna mipango**

Haya ni makosa ambayo inawezekana unayarudia kila mwaka inakufanya ubaki hapo hapo au kukufanya hatua zako ziwe kidogo.

Mipango ndiyo alama ya kwamba unasonga mbele au umebaki ulipo. Mipango inakutengenezea nidhamu ya matumizi sahihi ya rasilimali zako kama muda na fedha.

**2. Unaanzisha mambo halafu hufiki mwisho unaishia njiani**

Ili upate matokeo, lazima kuwe na mwendelezo wa mambo (consistency).

Kitendo cha kuanzisha jambo na kushindwa kulipa mwendelezo, kinafanya jambo hilo kukosa nguvu ya kuja baadaye kulikamilisha.

**3. Unaahirisha mambo.**

Tabia ya kuahirisha mambo (procrastination), ni moja ya tabia ya vikwazo vya mafanikio ya watu, kuahirisha ni kupanga na kila siku unasema nitatekeleza kesho.

Ukitaka mafanikio kwenye maisha, wekeza nguvu kwenye utafiti wa mambo na ukishaamua, anza maramoja utekelezaji.

Kwa kifupi, kuahirisha ni nguvu ya kurudisha nyuma ya mafanikio.

**4. Mwepesi wa kukata tamaa.**

Kukata tamaa ni adui wa mafanikio, kukata tamaa kunasababishwa na vikwazo njiani.

Vikwazo vinakufumba macho ya akili yako usione mwisho wa jambo, unahitaji kuona mwisho wa jambo tangu mwanzo, ili vikwazo vijapo, ushinde na kusonga mbele.

**5. Uvivu**

Uvivu ni kukosa nguvu ya kutekeleza jambo, uvivu ni kiunganishi cha tabia mbaya nyingine kama kuahirisha mambo, kufanya jambo kwa ulegevu, kufanya kwa viwango vya chini (sub standard), n.k.

**6. Hautimizi ahadi zako (you dont keep your promise) -**

“No commitment” kwenye mambo uliyopanga, hutekelezi ahadi zako, unapanga kuanza kujiendeleza kwa kusoma vitabu, lakini unakosa nguvu yakutekeleza, unapanga kuanza kufanya mazoezi, lakini unashindwa kutimiza.

**7. Huwezi kujizuia yaani ku – “sacrifice” raha za muda** ili **kufikia malengo ya muda mrefu (for the long-term goals)**

“Delay gratification” ni uwezo wa kujizuia kufanya mambo yanaonekana mazuri kwa sasa kwa ajili ya faida ya baadaye. Kwa mfano, unadhibiti hamu (appetite) yako kwa faida ya afya yako, unajinyima usingizi kwa saa kadhaa ili upate muda wa kusoma au unajinyima starehe kwa muda, kwa malengo makubwa ya maisha.

**8. Huna mtiririko wa mawazo yanayoweza kukupeleka kwenye mawazo (ideas).**

Mawazo yako yametawanyika, mara unawaza hili mara lile. Unawaza bila kuwa na lengo mahsusi (You are thinking nowhere).

**9. Uwezo wako wa kuwasiliana ni mdogo (poor communication)’**

Hali hii itakufanya ushindwe kuwa na mahusiano mema, jambo ambalo litakufanya ukose “connections”

Jifunze, anza sasa kutengeneza uwezo wako wa kuwasiliana na kujenga hoja zikaeleweka kwa watu.

**10. Kupenda sana usingizi**

**11. Kutoona mbali.**

**12. Kutokuwa na vipaumbele.**

**13. Mtazamo mbaya kwa maana ya “wrong focus”**

Unatazama zaidi matatizo yako kuliko unavyotazama malengo yako.

Moja kati ya uwekezaji mkubwa unaotakiwa kuufanya ni kushughulika na tabia zako, hasa kuondoa tabia kikwazo na kujenga tabia wezeshi. Msingi wa mafanikio uko kwenye tabia zako zaidi.

Maisha ni mchakato (process), hivyo jitihada zozote za kutafuta mafanikio kwa njia za mkato (shortcuts), -haziwezi kukupa ushindi utakaodumu.



Jarida hili haliuzwi

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

Uelekeo

# JARIDA Jungu Kuu

| Jumatano Desemba 13 - 19, 2023 |




# Rais Samia anavyotoa majibu sahihi...




UK. 12 & 13

Jamii

# Umasikini na maendeleo ya Tanzania - 5

**Na Dk. Felician Kilahama**

TUMSHUKURU Mungu kwa yote maana ndiye mwenye kuturehemu na fadhili zake kwetu ni za milele .

Hii ni Sehemu ya Tano na ya mwisho katika mwendelezo wa makala hii inayojadili masuala ya maendeleo katika taifa letu kwa kuzingatia utaratibu unaotumika kapima maendeleo na utajiri wetu kwa kutumia vigezo au viashiria vinavyotumiwa na mataifa tajiri.

Katika Sehemu ya Nne ya makala hii ilihitimishwa kwa kueleza umuhimu na upekee wa halmashauri zote nchini katika kuchochea maendeleo ya wananchi vijijini na mijini.

Mambo kadha wa kadha yameelezwa na kufafanuliwa tangu sehemu ya kwanza. Yapo masuala yanayostahili kutiliwa maanani katika shughuli za serikali kwa ujumla wake. Hivyo, ni vema kuwepo 'mapinduzi' mahususi katika sera na mitazano ya watunga sera na wanaofanya maamuzi.

Kwanza, pawepo na UTASHI MKUBWA WA KISIASA . Kwa kuzingatia utashi huo, mapinduzi ya kifikra yapelekee kujenga maadili mema na taifa kuwa na miiko mahususi pia kuweka mkazo kwenye uzalendo ili kuwatumikia na kuwajali wananchi badala ya ubinafsi na kujenga matabaka baina ya walio nacho" na wasio nacho .

Ili Watanzania tuweze kuumiliki uchumi kwa asilimia kubwa; tutake tusitake inatulazimu kufanya kazi kwa bidii na maarifa kwa faida ya kizazi hiki na vizazi vitakavyofuata.

Kwa sasa kinachogomba ni kukiri kuwa tu-maskini wakati halihalisi ni tofauti kwani vigezo vinavyotumika kuupima umaskini Tanzania haviendanu na uhalisia wetu.

Kadhalika, fikra za kuona mambo mengi hatuyawezi wakati tunaweza, siyo fikra sahihi. Tunakwama wapi na nini kinatukwamisha? Tukiyatambua hayo tuchukue hatua sahihi na kwa wakati bila kukawia.

Iwapo wengine walifanikiwa au wanafanikiwa, wakati walizaliwa na mwanamke kama sisi; hakuna sababu ya kusitasita. Malathani uchumi wa viwanda kumilikiwa kwa kiasi kikubwa na jamii ya nje au Watanzania wachache na kuendelea kupeleka malighafi nje ya nchi wakati huohuo kuagiza bidhaa zitokanazo na malighafi hizo kwa gharama kubwa, je, ni sahihi? Tujitathimini!

Maandiko Matakatifu yanatuasa kwamba hekima zijae kwa wingi ndani mwetu tusije "tukaangamia kwa kukosa maarifa".

Nanukuru: "Kwa maana watu wangu ni wapumbavu, hawajui: ni watoto waliopungukiwa na akili, wala hawana ufahamu, ni wenye akili katika kutenda mabaya, bali katika kutenda mema hawana maarifa" (Nabii Yeremiah 4:22).

Bila ya kuongozwa na Roho ya Mungu hakika taifa litazongwazongwa na mizozo isiyokuwa na maana na kushindwa kufanikiwa katika mambo yetu bila sababu za msingi.

Haipendezi kukubali masharti ya mataifa tajiri kwa kujiona kuwa wao ndiyo wenye haki zaidi katika sayari hii kuliko wengine. Mathalani, kukumbatia ushoga kwa minajili ya kupokea misaada ni sawa na kujitia kitanzi pia ni kiashiria cha kukosa au kudharau maarifa na mafundisho ya maandiko matakatifu.

Tanzania tunaweza, sina shaka na hilo, kinachotakiwa ni maamuzi sahihi hasa katika masuala muhimu kulingana na sera zilizopitishwa rasmi kitaifa na kuungwa mkono na watanzania wengi.

Tuangalie mambo ya msingi kama elimu na kazibili kwa kuwapatia vijana ujuzi toshelezi na kuwawezesha kuyamudu maisha bila kutegemea sana kuajiriwa baada ya kumaliza mafunzo husika. Nashukuru kuona serikali ya Awamu ya Sita ikiliangalia hilo katika mabadiliko ya sera na mitaala.

Cha msingi ni kwamba dhana hii, inatakiwa kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu ili tuweze kuwa na wataalamu mbalimbali wa stadi za kazi m kwa ngazi zote. Kama ni 'injinia' basi awe 'injinia' aliyeiva vizuri kinadharia na kimatendo.

Nihitimishe kwa kusema kwamba, miaka 62 ya uhuru, tumekuwa kama tunajifunza mara kwa mara. Tulipopata uhuru taifa liliazimia kuujenga uchumi imara utakaowanufaisha Watanzania wote. Tukaweka mikakati ya kufikia lengo hilo; ikiwa ni pamoja na kuhamasishana kupitia kaulimbiu kama Uhuru na Kazi; 'Ujamaa na Kujitegemea'; fanyakazi kwa bidii usiwe kupe ; ubepari/ukabaila ni unyama na kaulimbiu nyingine kadhaa.

Nia ilikuwa kuijenga jamii iliyoimara na yenye ari kubwa ya kujiletea maendeleo kwa kufanyakazi kwa bidii, haki na usawa bila kubaguana au kunyanyasana kwa misingi ya rangi, ukabila, udini; elimu na uwezo wa kifedha/mali nyingi na/au ubwanyenye/utwana.

Pamoja na hayo yote, tuliweza kufanikiwa kwa kujenga umoja wa kitaifa ulio imara na lugha ya Kiswahili ikawa nguzo kubwa katika kufanikisha suala hilo muhimu.

Baada ya wakoloni kuondoka tukaendelea na mfumo wa serikali za mitaa (Local Authorities) pamoja na vyama vya ushirika vya msingi pia vyama vikuu kama: Bukoba Cooperative Union (BCU); Kilimanjaro Native Cooperative Union (KNCU); Nyanza Cooperative Union (NCU) na kadhalika.




Taasisi hizo zilifanya kazi nzuri ya kuunganisha wakulima kwa kununua mazao husika na kutafuta masoko pamoja na kuwapatia huduma za ugani na kuwapatia pembejeo mbalimbali hivyo, kwa kiasi fulani, wakulima walinufaika.

Ikatokea serikali ikavunja vyama vya ushirika na kuanzisha mfumo wa Bodi za Mazao mfano za Kahawa; Pamba au Korosho. Mabadiliko hayo pia yaliendana na kuondoa mfumo wa serikali za mitaa na kuanzisha utendaji mbadala.

Hivyo, wilaya zikaongozwa na Wakurugenzi wa Maendeleo (District Development Directors-DDDs) na wakuu wa wilaya wakaitwa Area Commissioners badala ya District Commissioners (DCs). Mabadiliko hayo hayakudumu kwa kipindi kirefu, Serikali ikarejesha mfumo wa awali wa halmashauri, madiwani wakawepo pamoja na watendaji wakiongozwa na wakurugenzi watendaji (District Executive Directors (DEDs)) lakini wakuu wa wilaya wakabaki hivyo. Vilevile, ikaundwa wizara ya kuratibu shughuli zote za mikoa na serikali za mitaa ambayo ni Wizara ya Tawala za Mikoa, na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Kadhalika, serikali kwa awamu zote (sasa ya sita) kumekuwepo na kubadilishwa baadhi ya wizara, wakatimwingine kufuta na/au kuunda mpya. Mathalani, Wizara ya Mipango na Tume ya Mipango; ni vyombo vya utendaji ambavyo vimekuwepo na kufanya kazi. Kurejeshwa Wizara hiyo ni ishara kuwa yapo mapungufu katika utendaji wa serikali kuhusu kupanga, kutekeleza na ufuatiliaji.

Sasa ni wakati mwafaka wa kujitathimini ipasavyo kwa ajili ya kuondoa mapungufu na kujiwekea mikakati mipya ya kutuwezesha kusonga mbele kwa kasi zaidi na kwa faida ya wengi mijini na vijijini.

Kiini cha makala hii ni kuhusu utaratibu unaotumika kupima umaskini na maendeleo ya Tanzania. Tujiulize, tunapoambiwa Tanzania ni maskini je, ni sahihi? Au kutangaziwa kwamba Afrika ni maskini sana, je, halihalisi ni hivyo? Neno maskini humaanisha kutokuwa na kipato cha 'kutosha'. Je, Tanzania ndivyo hali ilivyo? Na kipato cha kutosha maanake nini? hilo ni neno linalotokana na neno tosha ikimaanisha kiwango cha kuridhisha au kinachohitajiwa.

Kulingana na mazingira yetu, Watanzania tuko 'poa' na kuishi maisha yanayoashiria kuwa hatuko 'maskini' kama wanavyotafsiri. Isitoshe, hata mataifa yaliyoendelea (matajiri) walichangia sana kuzorotesha maendeleo ya nchi za Afrika hadi kudorola kiuchumi kupitia "nguvukazi" kutoka Afrika kuhamishiwa kwao.

Vilevile, rasilimali nyingi kutoka Afrika zilihamishwa na wakoloni wakazipelekwa kwao kwa minajili ya kujiendeleza wenyewe kiuchumi na kijamii.

Pamoja na Afrika kuwahuru, bado kwa njia moja au nyingine, kuna viashiria vya kuwepo ukoloni mamboleo na kwa njia hiyo bado rasilimali kutoka Afrika zinahamishwa kwenda mataifa mengine husunani, mataifa tajiri kupitia faida kubwa wanazopata kutokana na fursa za uwekezaji pamoja na kusafirisha malighafi kutoka barani Afrika.

Mathalani, madini, rasilimali misitu na wanyamapori, wataalamu muhimu (brain-drain) pamoja na mikataba mikubwa ya miradi ya maendeleo kutekelezwa na makampuni ya nje badala ya makampuni ya hapa nchini au ya Afrika Mashariki, kuwa mstari wa mbele (tujitathimini tuchukue hatua sahihi).

Kwa kuwa Tanzania tunahitaji kujiletea maendeleo, ni lazima tufanyekazi kwa bidii na kujituma bila kuchoka; wakati huohuo tukizingatia masilahi mapana ya taifa letu.

Ni vema tukajitathimini tulipotoka, tupo wapi na mwelekeo wetu sahihi ni upi? Vyombo kama Taasisi ya Taifa ya Takwimu (NBS); Kamisheni ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH); Taasisi za Utafiti, na Vyuo Vikuu; na Watafiti wengine katika sekta-binafsi (kama wapo) kwa pamoja tuunganishe nguvu tuhakikishe taifa lina vigezo vyake vya kupima maendeleo yake bila kutetereka: inawezekana, tunaweza, tusonge mbele. Tusikubali kujioni sisi ni maskini maana maneno yanaumba tunaweza tukasonga mbele zaidi ya sasa. Inawezekana kwake aaminiye.



Hamisi Kibari

## TUKUBALIANE KUTOKUBALIANA

Simu: 0758143457

# ‘Hata watunzi wa riwaya wanaiba kazi za wengine’

NINAWAJUA watu wengi ambao ni wasomaji wa riwaya mashuhuri nchini pamoja na vitabu vingine vya ujuzi na maarifa lakini miongoni mwa wako watatu mashuhuri zaidi.

Kusema hivi si kwamba kwenye riwaya hakuna maarifa la hasha, pengine kwenye riwaya mtu akapata maarifa kwa wepesi zaidi kama mwandishi amefanya utafiti wa hoja zake kwani msomaji anakuwa anaburudika na mkasa huku akijifunza kitu, wazungu wanaita Edutainment (education and entertainment).

Hao wasomaji watatu maarufu zaidi wa riwaya ninaowajua mimi ni Buinda Mjungu wa pale Arusha, Salim Aljabri wa Dar es Salaam na Peter Chapusa ambaye makazi yake yako Bagamoyo.

Hawa watatu Mungu amewajaalia sana uwezo wa kusoma riwaya na ni wapenzi wakubwa wa watunzi. Takribani kila kitabu kipya cha riwaya kinachotoka wanakitafuta, wananunua na kukisoma. Yaani ni watu ambao katika matumizi yao ya kila siku kuna bajeti ya kitabu!

Mimi nilikuwa siwajui wala wao hawanijui lakini kwa kutoa vitabu viwili, ghafla nikawa swahiba wa wote watatu, Alhamdulillah.

Hivi karibuni, katika safu hii niliandika makala nikiwanyooshea kidole baadhi ya watengeneza filamu wa Tanzania ambao wameshindwa kuboresha filamu zao kutokana na kutotilia maanani chanzo cha filamu nzuri, yaani hadithi. Hata hivyo, makala hiyo haikupita hivihivi bila mmoja wa hawa wasomaji wakubwa wa riwaya nchini kueleza dukuduku lake.

Katika makala ile nilisema kwamba kampuni ya Azam ambayo imetangaza kuanza kupokea filamu mwezi Januari, inaweza isipate filamu nzuri za kiwango cha kimataifa kama waandaji wa filamu tulio nao wataendelea kutotilia maanani utafutaji wa hadithi nzuri.

Nikashauri watengeneza filamu kushirikiana na watunzi mahiri wa riwaya tulio nao nchini kwa maana ya kununua hadithi zao kwa mikataba maalumu ili watengeneze filamu ‘bomba’ zaidi.

Nikafafanua kwamba ingawa kitu cha kwanza kinachofanya filamu nzuri ni uzuri wa kisa (hadithi), kutokana na uzoefu wangu watengeneza filamu wa Tanzania wamekuwa hawatilii maanani kabisa kipengere hicho muhimu.

Kwamba kutokana na wengi wao kutokuwa watunzi, wamekuwa wakitengeneza filamu zao kwa hadithi za ‘kubabia’ kwa maana ya kuchukua hadithi za watu wengine, na kubadilishabadilisha hapa na pale na kujifanya wametunga wao!

Kwa kufanya hivyo nikasema mara nyingi hawapati kisa kilichonyooka kutokana na jitihada zao za kubadilibadili kisifanane kabisa na kisa ‘walichoiba’.


Nilisema ingawa watunzi wa Tanzania wamekuwa wakikumbana na wizi wa hadithi zao kutengenezwa filamu, lakini pia watunzi wa nje hasa wa Nigeria ndio kwa kipindi kirefu wameibiwa sana mawazo yao.

Hata hivyo, mmoja wasomaji wakubwa wa riwaya, Chapusa aliposoma hiyo makala aliniambia kwamba kile nilichowanyooshea kidole watayarishaji wa filamu za ‘kibongo’, pia kinafanywa na watunzi wa riwaya wa Tanzania!

**CHAPUSA NI NANI**

Kwanza tusimame kidogo nimwelezee huyu Chapusa ni mtu wa aina gani, pengine utaona ni kwa nini maoni yake yanakuwa muhimu.

Nilikutana naye kwa mara ya kwanza kwenye moja ya mikutano iliyoandaliwa na Umoja wa Waandishi wa Riwaya Wenye Dira (UWARIDI), ingawa kabla ya hapo nilikuwa nimeshasikia habari na sifa zake. Kwa hiyo UWARIDI wanamtambua na ndio maana wanamwalika kwenye miktano yao muhimu.



Mwandishi wa makala haya akiwa na mmoja wa wasomaji mashuhuri wa riwaya nchini, Peter Chapusa (kushoto)

Katika kuzungumza naye niligundua kwamba huyu mwamba akisoma hadithi yako, anaweza kuihadithia vizuri kuliko hata wewe mwenyewe mtunzi na huwajua kwa majina hata wahusika wadogowadogo!

Aliniambia katika mazungumzo yetu mafupi kwamba, ukiacha vitabu vichache alivyowahi kuazima, pale nyumbani kwake Bagamoyo ana vitabu zaidi ya 400 kwenye maktaba yake nyumbani.

“Hata sasa hivi tukienda nyumbani Bagamoyo nitakuingiza kwenye chumba na nitakuonesha vitabu vya riwaya zaidi 400 nilivyo navyo,” alisema kwa kujiamini.

Aliniambia alianza kupenda riwaya mwaka 1983 akiwa darasa la nne baada ya kuvutiwa sana na kitabu cha Operesheni Sukuma Namba 8, utunzi wake Kassim Kassam.

Alisema akiwa sekondari, walimu wa fasihi walipokuwa wanawapa vitabu vya kusoma darasani, alijikuta kila mara akiwa na kibarua cha kusoma na kisha kuwasimulia wenzake kilichomo kwenye kitabu, maudhui, wahusika, taharuki na mengine kwa kifupi na hivyo alikuwa msaada mkubwa kwa wanafunzi wake.

Tuishie hapa uhusu Chapusa lakini kuna siku nitamtafungia safari Bagamoyo ili niandike wasifu wa mtu huyu wa ajabu kidogo kwangu kwa kirefu zaidi, InshaAllah.

**WIZI WA KAZI ZA WENGINE**

Chapusa aliniambia kwamba kuna watunzi kadhaa wa Tanzania, wakiwemo ambao wanaonekana kuwa maarufu, wamebobea sana kwenye kuchukua hadithi za watunzi wenzao wa Tanzania na kuzibadilisha kidogo.

Chapusa anasema amekuwa akisikitishwa sana na tabia ya watunzi hao wa Tanzania kuiba kazi za Watanzania wenzao bila aibu, mchana kweupe.

Huku akiwataja majina, mmoja baada ya mwingine na kitabu alichoiba hadithi yake, Chapusa anasema kwamba baadhi yao huwa anawapigia simu na kuwasema.

Anasema kuna mmoja kachukua kitabu cha mtunzi mmoja ambaye pia ni mwanamuziki takribani kila kitu isipokuwa kabadili majina tu.

Akasema mmoja wa watunzi wenye vitabu vingi sokoni (si mwanachama wa UWARIDI) alimpigia simu akimtaka amrudishie fedha zake baada ya kununua ‘kitabu chake kipya’ na kugundua kisa kizima kilishaandikwa na mtu mwingine!

“Tena hiyo haikuwa mara ya kwanza kugundua kwamba ameandika riwaya lakini ‘kakopi’ hadithi za mtu mwingine. Na huyu bwana anaiba sana hadithi za Marehemu Ben Mtobwa. Anadhani wengi hawatajua lakini kuna akina sisi tunajua. Ninaweza nikakuletea kitabu cha Ben Mtobwa na hicho chake uone kama kuna tofauti.

“Lakini alinishangaza kuhusu majibu yake nilipomwambia ukweli kwamba ameiba kazi ya Mtobwa. Alisema eti huwa anaandika kwa kujifurahisha tu. Yaani unaiba hadithi ya mtu, unachapa kitabu kwa jina lako na kukitangaza sana kwenye makundi ya Whatsapp kwa kujifurahisha tu. Haiwezekani!”

**WEZI WASHUGHULIKIWE**

Hii inasikitisha sana kuona kwamba kumbe tuna watunzi wezi, wakitamba na kazi za wenzao (plagiarism) huku jamii ambayo haina bahati ya kusoma vitabu vingi kama ya Chapusa ikiwa haielewi kinachoendelea na badala yake kuwamwagia sifa chungu mzima hawa wezi.

Nimekuwa ninajiuliza kama ingekuwa busara mamlaka zinazolinda kazi za waandishi (intellectual properties) zikawatumia watu kama Chapusa kukamata kazi za wizi sokoni ili kukomesha aina hii ya wizi.

Sijui kama wahusika katika Chama cha Hakimiliki Tanzania na Haki za Jirani (COSOTA) kilichoanzishwa chini ya kifungu cha 46 cha Sheria namba 7 ya mwaka 1999 wakisoma makala haya wanaweza kuja na ufumbuzi wa wizi huu hata kama mtu hajasajili kazi yake katika chama kicho?

Hivi tangu chama hicho kianzishwe kimeshakamata wezi wangapi wa kazi za wengine?

Kwangu, mtu anayeiba kazi ya mwingine na kuandika kitabu kwa jina lake au kutengeneza filamu ni mwizi kama wezi wengine hata kama kamwibia Mnigeria na ndio maana COSOTA inapaswa kulinda pia haki za jirani.

Mwizi mahala panapomstahili ni jela.

Siasa

# Samia anavyotoa majibu sahihi kwa wahafidhina

## ■ Hakika kazi inaongea



**Na Hamid Yassin**

TANGU aingie madarakani Machi 19, 2021, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk Samia amekuwa akijipambanua kama kiongozi anayeongoza kwa kutumia nguzo nne ambazo zinalenga kuliunganisha Taifa la Tanzania katika nyanja zote zikiwemo za kisiasa, kijamii, kiuchumi na kiutamaduni.

Katika toleo maalumu la Uhuru, nguzo hizo ziligusiwa lakini makala hii inajaribu kuzifafanua kwa kina na hasa kwa namna anavyowafunga midomo wahafidhina. Uhafidhina ni falsafa ya kisiasa inayolenga kulinda, kusimamia na kufuata mila, desturi na taratibu za jamii au taifa fulani.

Uhafidhina (coservativism) ni hali ya kutotaka sana mabadiliko na hapa Tanzania, moja ya chama cha siasa chenye mrengo huo ni Chama Cha Damokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

**DEMOKRASIA**

Katika kulifanya taifa kuwa moja lenye kufurahiwa na kila Mtanzania, Rais Samia amekuwa akitumia Falsafa ya "R" nne zinazotokana na maneno ha Kiingereza, ambazo ni Maridhiano (Reconciliation), Ustahamilivu (Resilience), Mageuzi (Reforms) na Ujenzi Mpya (Rebuild).

Mwenye macho haambiwi tazama, kila Mtanzania amejionea mwenyewe namna Rais anavyoendelea kufanya maridhiano katika nyanja ya siasa ambapo kwa nyakati tofauti amekutana na viongozi wa vyama vya siasa na kufanya nao mazungumzo yenye lengo la kujenga umoja wa kisiasa nchini.

Miongoni mwa viongozi aliokutana nao ni pamoja na Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, viongozi wa vyama vya ACT Wazalendo, Chama cha ADC, Chama cha Wananchi (CUF) na pia viongozi wa Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD).

Katika mikutano yote hiyo, Dk. Samia alikuwa akisisitiza umuhimu wa kushirikiana ili kuijenga Tanzania yenye kuaminiana na kuheshimiana kwa misingi ya haki.

Akizungumza kuhusu suala la maridhiano, Mwenyekiti wa Chadema, Mbowe alielezea umuhimu wa kuondoa uhasama wa kisiasa pamoja na kusameheana.

"Umeonesha njia kwa taifa lako namna tunavyopaswa kuwa, Rais Samia na falsafa yako ya R nne katika kuijenga nchi yetu Tanzania umedhamiria kusameheana ili kwa pamoja tujenge taifa lenye uhuru, haki, demokrasia, na maendeleo ya watu wote," alinena Mbowe bila kupepesa macho!

Machi 8 mwaka huu, Rais Samia aliwashangaza wengi pale alipohudhuria Kongamano la Baraza la Wanawake la Chadema (BAWACHA) na kutoa hutuba iliyowavutia siyo wanasiasa na wanaharakati bali watu wengi ndani na nje ya nchi.

Kitendo cha kuhudhuria mkutano wa kisiasa ulioandaliwa na chama kikuu cha upinzani ndani ya nchi yake, ni cha kihistoria si kwa Tanzania tu bali karibu bara zima la Afrika!

Hotuba yake ile ilikuwa na maneno mengi ya busara yakiwemo ya kuwaasa viongozi wa Chadema kujiepusha na wahafidhina.

"Nimekuja hapa lakini naelewa kuna baadhi ya Wanachadema hawakufurahishwa na jambo hili, wanasema kwa nini umemwita rais kwenye jukwaa hili, Mwenyekiti (Mbowe) sasa ujue hata huku kuna wahafidhina, wengine wanasema Mbowe amelishwa asali huku wao wanakimbilia nje ya nchi na kung'ang'ania huko; Kwa hiyo Mwenyekiti uelewe huku kuna wahafidhina na kule kwangu pia wapo," alinena Dk. Samia kwenye kongamano lile.

Alisisitiza kwamba lazima nchi ijenge amani na utulivu ili ipate maendeleo; "Ulipotoka jela walitaka kujua ulifuata nini Ikulu, lakini nafurahi uliwajibu hutaki turejee kule! Wahafidhina watatuelewa maendeleo yanapokuja, bila amani na utulivu hakuna maendeleo."

Kwa kweli haya ananayohyafanya Rais ikiwemo kuondoa kodi za uonevu kupitia mifumo ya hakijinai, kuimarisha uhuru wa kujieleza, na kurejesha haki ya kufanya mikutano ya siasa na watu kukusanyika, hakika anapaswa kupongezwa.

**MIRADI YA KIMKAKATI**


Miradi yote mikubwa ya kimkakati iliyoanzishwa au kuendelezwa na awamu ya tano, naye pia anaiendeleza kwa kasi nzuri huku wahafidhina wengi wakiwa hawaamini macho yao!

Ujenzi wa reli ya mwendo kasi (SGR) hayati Magufuli aliacha ukiwa chini ya asilimia 90 kati ya Dar es Salaam na Morogoro, lakini kipande hicho chini ya Dk. Samia kimekamilika, baadhi ya mabehewa yameshafika, kichwa kimoja cha mabehewa hayo (injini) kimepakuliwa mwezi huu bandarini na kinachosubiriwa sasa ni majaribio ya safari kati ya Dar na Moro!

Ile falsafa yake ya 'Kazi iendelee', akimaanisha kuendeleza yote mazuri ya mtangulizi wake haikuwa ya kinafiki; kwani sasa vipande vyote vilivyobaki vya mradi huo vimeshasainiwa na hivi sasa makandarasi wako maeneo ya kazi wakiwajibika.

Wakati utiaji saini wa ujenzi wa kipande cha SGR Tabora-Kigoma mwishoni mwa mwaka jana, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa alisema ujenzi wa SGR katika vipande vyote unaendelea vizuri.

Kadogosa alibainisha kuwa, Serikali ya Rais Samia imefanikiwa kuendeleza ujenzi huo ambao mpaka wakati ule



ujenzi kutoka Dar es Slaam hadi Morogoro ulifikia asilimia 97.67, Morogoro hadi Makutupora ulikuwa asilima 91.32, Makutupora mpaka Tabora ulishafika asilima 3.26, Tabora-Isaka (asilima 0.49) na Isaka-Mwanza ulishafika asilimia 19.70. Kumbuka takwimu hizi ni za mwaka jana, hivyo ujenzi wa reli hiyo hadi sasa utakuwa umefika mbali zaidi.

Mradi mwingine wa kimkakati ni ujenzi wa Bwawa la Julius Nyerere (JNHPP) la kuzalisha umeme wa maji Mto Rufiji. Wakati anazindua ujazaji maji wa bwawa hilo Desemba 22 mwaka jana, Rais Samia alisema alikuta ujenzi wa mradi huo ukiwa asilimia 37 wakati anaingia madarakani, lakini mpaka siku ile ya ujazaji maji ujenzi wake ulikuwa umefikia asilimia 78.68. Na Mkandarasi ameahidi hadi kufika Aprili mwaka 2024 mradi utakuwa umekamilika na utakabidhiwa rasmi serikalini!

Miradi mingine ya kimkakati inayoendelea kwa kasi ya kimbunga ni pamoja na ujenzi wa Daraja refu la Magufuli (Kigongo Busisi Mwanza), ununuzi wa ndege mpya za Shirika la Ndege nchini (ATCL), bomba la mafuta kutoka Houma, Uganda hadi Tanga, uboreshaji wa bandari ambayo sasa imepata mwekezaji, kjiwanja chandege cha msalato na miradi mingine lukuki.

### DIPLOMASIA YA KIMATAIFA

Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Dk. Samia imerudisha uhusiano mzuri sambamba na kujiimarisha kwenye ramani ya dunia katika nyanja ya diplomasia ya kimataifa.

Hii ni tofauti na hali aliyoikuta wakati akishika hatamu za uongozi wa nchi yetu ambapo uhusiano wetu na nchi nyingine kimataifa ulikuwa wa kusuasua.

Rais Samia katika uongozi wake, ametumia mikakati mbalimbali ya utekelezaji wa diplomasia ya kimataifa kwa lengo sio tu la kukuza uhusiano bali pia kukuza uchumi wa nchi kwa kuvutia uwekezaji, biashara na utalii.

Baadhi ya mikakati ambayo Rais Samia anaitumia kama nyenzo muhimu ya kukuza na kuimarisha diplomasia ya Tanzania duniani kote ni pamoja na ziara za viongozi wa kitaifa nje ya nchi. Ziara ni moja ya nyenzo muhimu za utekelezaji wa diplomasia.

Katika kipindi cha karibu miaka mitatu ya uongozi wake, Rais Samia pamoja na viongozi wenzake, wakiwemo Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango; Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi; Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa Majaliwa; Mawaziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, tangu wakati wa Liberata Mulamula, Dk Stergomena Tax hadi wa sasa hivi, January Makamba na mawaziri wengine kadhaa wamefanya ziara katika nchi mbalimbali duniani kukuza demokrasa ya kisiasa na uchumi.

Kupitia ziara hizi, mikataba na hati za makubaliano zaidi ya 90 imesainiwa kati ya Tanzania na nchi hizo katika maeneo ya uwekezaji, biashara, utalii na ujenzi wa miundombinu.

### THE ROYAL TOUR

Royal Tour ilikuwa fursa ya kimkakati ya kuitambulisha Tanzania kimataifa, kuvutia uwekezaji nchini, na kutangaza utalii ambapo katika kipindi cha kuelekea mwaka wake wa tatu imefanikiwa kushawishi watalii mbalimbali wa ndani na nje ya nchi kutembelea mbuga zetu na vivutio vingine vya kitalii.

Wawekezaji na mawakala wa utalii zaidi ya 30 kutoka katika nchi za Marekani, Ufaransa na Lithuania walitembelea Tanzania ili kujifunza na kujionea vivutio mbalimbali vya utalii kwa lengo la kuvitangaza katika nchi hizo.

Kutokana na juhudi hizo, katika kipindi cha mwaka 2022 idadi ya watalii walioitembelea Tanzania imeongezeka kwa asilimia 57.7 kutoka watalii 922,692 mwaka 2021 hadi kufikia watalii 1,454,920 mwaka 2022.

Watalii hao wameongozwa na taifa la Marekani,Ufaransa, Ujerumani, Uingereza, Poland, Italia, India, Uholanzi, Hispania na Jamhuri ya Czech.

Kwa upande wa nchi za Afrika watalii wengi wametoka Kenya, Burundi, Zambia, Malawi, Rwanda, Afrika Kusini, Uganda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Zimbabwe na Msumbiji.

Pamoja na ongezeko la idadi ya watalii wa kimataifa, utalii wa ndani pia umeendelea kuimarika nchini ambapo katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2022, idadi ya watalii wa ndani waliotembelea maeneo ya hifadhi zetu imeongezeka kwa asilimia 199.6 kutoka watalii 788,933 mwaka 2021 hadi kufikia watalii 2,363,260.

Aidha, sambamba na ongezeko hilo, sekta ya utalii nchini imefanikiwa kupata tuzo mbalimbali za kimataifa zikiwemo za Tanzania kuwa kituo bora cha utalii Afrika (Safari Bookings.com), Tanzania kuwa kituo bora cha kutembelea Barani Afrika (New York Times) na Ngorongoro imetajwa kuwa ni eneo bora duniani na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti imetajwa kuwa Hifadhi bora katika Afrika.

Aidha, kupitia kazi kubwa iliyofanywa na Dk. Samia, katika kipindi hiki cha miaka miwili na nusu ya uongozi wake wawekezaji kutoka Taifa la Bulgaria wanakusudia kujenga hoteli nne zenye hadhi ya nyota tano ambazo zitaendeshwa na Kampuni ya Kempinski katika Hifadhi za Taifa za Serengeti, Manyara, Tarangire na Hifadhi ya Ngorongoro.



Katika kipindi hiki Tanzania imekua mwenyeji wa mikutano na maonesho makubwa ya Kimataifa ya Utalii yaliyofanyika nchini ukiwemo Mkutano wa 65 wa Shirika la Utalii Duniani Kamisheni ya Afrika (65th UNWTO-CAF Meeting) uliofanyika Oktoba, mwaka 2022 Jijini Arusha.

Mkutano huo ulifanyika sambamba na Jukwaa la Uwekezaji, Jukwaa la Utangazaji Utalii na Uzinduzi wa Mwongozo wa Uwekezaji wa Tanzania (UNWTO Investment attraction).

Katika kuhakikisha kuwa Sekta ya Utalii inaendelea kuimarika, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Dk. Samia imeimarisha miundombinu ya utangazaji Utalii kupitia matumizi ya Tehama.

Wizara ya Maliasili na Utalii, kupitia Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) imenunua vifaa vya kisasa vya kituo cha kutolea taarifa za utalii kidijiti (Digital Command Center) ili kuwezesha utangazaji wa utalii kwa kutumia mitandao ya kijamii na tovuti.

Aidha, Serikali imejenga na kukarabati barabara zenye urefu wa kilomita 2,383.12 katika maeneo ya hifadhi za taifa, mapori ya akiba, tengefu na misitu ya hifadhi ya mazingira asilia; viwanja vya ndege nane (8) katika Hifadhi za Taifa za Nyerere, Tarangire, Mkomazi , Saadani na Mapori ya Akiba ya Maswa na Ziwa Natron.

### MADINI

Rais Dk. Samia ameendelea kuisimamia na kuiongoza ipasavyo sekta ya madini kama ambavyo Kifungu cha 5 (1) cha Sheria ya Madini kinavyoainisha na hivyo kuifanya sekta hiyo kuendelea kuchangia vyema taifa letu kiuchumi na kimaendeleo.

Kifungu hicho cha sheria kinaeleza kwamba, mali yote na udhibiti wa madini yote ndani, chini au juu ardhi yoyote, vijito, njia za maji kote Tanzania, eneo ndani ya mipaka ya bahari, rafu ya bara au eneo la pekee la kiuchumi ni mali ya Jamhuri ya Muungano wa chini ya udhamini wa Rais kwa niaba ya Watanzania.

Kutokana na usimamizi huo thabiti, katika kipindi hiki akiwa madarakani, mchango wa sekta ya madini katika pato la taifa umeendelea kuongezeka kutoka asilimia 6.7 mwaka 2020 hadi asilimia 7.3 mwaka 2021.

Kwa vipindi vya robo mwaka vya 2022, mchango wa sekta umekuwa ukiimarika, ambapo katika kipindi cha robo ya kwanza Januari hadi Machi ulikuwa asilimia 7.8, robo ya Aprili hadi Juni asilimia 8.3 na robo ya tatu ya Julai mpaka Septemba mchango wa Sekta umefikia asilimia 9.7.

### UUZAJI WA MADINI NJE YA NCHI

Katika kipindi hiki kifupi Rais Samia madarakani sekta ya madini imeendelea kuongoza kuchangia mapato ya fedha za kigeni kutokana na mauzo nje ya nchi ambapo mwaka 2021 ilichangia asilimia 45.9 ya mauzo yote.

Aidha, mwaka 2022, jumla ya vibali 10,318 vya kuuza madini nje ya nchi vilitolewa vyenye thamani ya dola za Marekani milioni 3,240.35 ikilinganishwa na vibali 5,526 vilivyotolewa mwaka 2021 vilivyokuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 3,046.23.

### UKUSANYAJI WA MADUHULI

Makusanyo ya maduhuli kutokana na madini yameendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka. Mwaka 2020/21 zilikusanywa shilingi bilioni 585.2, mwaka 2021/22 shilingi bilioni 624.6. Aidha, katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2022 jumla ya shilingi bilioni 353.4 zilikuwa zimekusanywa.

Katika miaka hii, Serikali imefanya marekebisho mbalimbali katika Sheria ya Madini Sura 123 na kanuni zake kupitia Sheria ya Marekebisho Mbalimbali, Na. 3 ya Mwaka 2022. Marekebisho hayo ni pamoja na kuanzisha leseni mpya ya uchenjuaji mdogo wa madini (Primary Processing Licence).

Hii ni kumpa Waziri mamlaka ya kurejesha serikalini maeneo ya leseni za madini zilizofikia ukomo; kuipa Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini (GST) mamlaka ya kisheria ya kufanya utafutaji wa madini wa kimkakati; kuweka muda wa uhuishaji wa leseni za utafutaji wa madini (Prospecting Licence) wa kipindi cha pili; na kuweka ukomo wa umiliki wa leseni ndogo ya uchimbaji (Primary Mining Licence) na kuanza shughuli za uchimbaji baada ya kupewa leseni.

*Itaendelea.*

Jamii

# Sawa Nape, Serikali isifumbie macho wahuni mitandaoni

**Na Hamid Yassin**

NAUNGA mkono uamuzi wa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia, Nape Nnauye, kwamba kwa mujibu wa sheria za nchi, Serikali itachukua hatua kwa wale wote waliohusika kutangaza uvumi wa kifo cha Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, kwenye mitandao ya kijamii.

Waziri Nape alisema hayo Desemba 10, mwaka huu kupitia akaunti yake ya X (zamani Twitter) saa chache baada ya Dk. Mpango kuwataka Watanzania kutumia vizuri mitandao ya kijamii na kuachana na kuzusha habari za uongo.

"Pole sana Mhe. Makamu wa Rais. Tumekusikia; kwa kuwa tuna sheria zinazoelekeza mitandao itumike vizuri na kwa kuwa tuna taasisi na watu wa kusimamia sheria hizi, bila kuathiri uhuru wa watu.

TUTACHUKUA HATUA kutokomeza matumizi haya mabaya ya mitandaoni. Naamini wote watatuelewa!" amesema Nape.

Ameelekeza vyombo vyote vinavyohusika kuchukua hatua ili iwe mfano na kujenga jamii inayoheshimu uhuru wa kila mtu.

"Uhuru wowote unapoingilia uhuru wa mwingine, ni uvunjaji wa sheria, kamwe hatuwezi kujenga jamii inayoona hilo jambo ni la kawaida," aliandika Waziri Nape.

Dk. Mpango hakuonekana hadharani kwa takribani mwezi mmoja, jambo ambalo baadhi ya watu walilichukulia kama fursa ya kuanzisha minong'ono kisha kuzusha uvumi kwamba alikuwa anaumwa huku wengine wakienda mbali zaidi kwa kudai amefariki dunia!

Mwenyewe Makamu wa Rais amesikitishwa sana na suala hili la kuzushiwa kifo akisema ni la pili kumtokea, kwani Oktoba 20, mwaka 2020, wazushi hao walifanya hivyo hadi kusababisha dada yake aanguke na kuzirai baada ya kusikia taarifa hizo potofu.

"Unajua ukisema huyu mzee amekata moto huku wengine wakiweka picha yangu iliyochongwa na mshumaa unawaka, haipendezi. Rais sisi viongozi ni binadamu tuna watoto, wajukuu, familia, marafiki na wafanyakazi wenzetu, hivyo kufanya hivyo inaweka taharuki kubwa, alinena kwa masikitiko Dk. Mpango.

> **Pole sana Mhe. Makamu wa Rais. Tumekusikia; kwa kuwa tuna sheria zinazoelekeza mitandao itumike vizuri na kwa kuwa tuna taasisi na watu wa kusimamia sheria hizi, bila kuathiri uhuru wa watu. TUTACHUKUA HATUA kutokomeza matumizi haya mabaya ya mitandaoni. Naamini wote watatuelewa!**

Si unafiki kusema kwamba Watanzania ni hodari kwa uongo na uzushi si tu barani Afrika, bali wanaweza kuongoza duniani.

Katika miaka ya themanini na tisini, Jiji la Lagos nchini Nigeria, lilisifika kwa uzushi, uongo kwa kisingizio cha wahitimu wa vyuo vikuu nchini humo kukosa ajira serikalini au kwenye mashirika na kampuni binafsi.

Wasomi hao waliokosa ajira serikalini, walijiingiza kwenye shughuli za utapeli ambapo walifanikiwa kuutekeleza kwa weledi mkubwa kutokana na elimu yao ikiwemo hili la kuzusha uvumi na kisha kuusambaza!

Hali hii sasa imeanza kujikita kwa kasi ya ajabu nchini mwetu tangu Serikali iliporuhusu mitandao ya kijamii. Mitandao hii imedhihirisha kile kinachoitwa uzushi na uongo uliovuka mipaka kutokana na kila mara kuzusha mambo ambayo kama hayatadhibitiwa, yanaweza kuiingiza nchi kwenye mitafaruku na machafuko.

Kabla sijaendelea zaidi, niweke wazi kwamba kuna aina mbili za mitandao hapa nchini, ile ya kimataifa kama vile Facebook, Instagram,

Twitter (X), WhatsApp na mingine kadhaa, lakini pia ipo ambayo ni ya hapa nchini, yaani imesajiliwa Tanzania na kuwa chini ya Mamlaka wa Mawasialiano Tanzania (TCRA) kama ule wa Jamii Forum.

Watanzania wamekuwa 'vichaa' kwa mitandao hii ya kijamii ya ndani na nje, kiasi kwamba hivi sasa kila siku wanalalamika gharama za mabando ya mitandao (internet) kupanda kwa kasi wakichelea kukosa uhondo wa mitandaoni ukiwemo wa umbeya na haya ya uzushi wa kila aina.

Wapo wachache wanatumia vizuri mitandao hii ya kijamii na kujiingizia vipato vya kutosha vya kuendeshea maisha yao. Hawa ni kama wale wanaofungua akaunti kwa madhumuni ya biashara za mitandaoni, wengine wameanzisha Televisheni za 'Online' na kadhalika.

Tukumbuke kwamba Rwanda iliingia kwenye ghasia zilizosababisha kutokea mauaji ya kimbari mwaka 1994 kutokana na matumizi mabaya ya masafa ya mitandao hiyo na baadhi ya vyombo vya habari kusambaza uzushi uliotopea na kusababisha mauaji yale.

Sasa muda mrefu tangu mitandao ya kijamii ijikite kwenye kuzusha uvumi wa kila aina hapa nchini.

Lakini Ilianza kukithiri katika kusambaza uongo wa hatari tangu enzi ya Serikali ya Awamu ya Tano ambapo kuna wakati ilipodai kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati huo , Dk. Samia Suluhu Hassan, alikuwa haelewani na hayati Rais Dk. John Magufuli.

Mitandao hiyo, ambayo maudhui yake yalinukuliwa na baadhi ya vyombo vingine vya habari vya hapa nchini, ilidai kuwa Makamu huyo wa Rais alikuwa ameandika barua ya kujiuzulu wadhifa wake huo, kitendo ambacho iwapo kingekuwa ni kweli, kingeiingiza nchi kwenye balaa la kutoweka kwa utulivu, amani na umoja wetu.

Aidha, mitandao hiyo iliwahi kuzusha habari za upuuzi kwamba hayati Dk. Magufuli alimtosa mtangulizi wake, Rais mstaafu wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete eti kisa alimkalia kooni kwenye serikali yake!

Hakuna ubishi kwamba mitandao hii imeamua kuwa mbadala wa vile vyama vya upinzani vilivyobobea katika kuzua taharuki na sintofahamu kwenye jamii yetu.

Nasema hivi kwa sababu uzushi mwingi kwenye mitandao hiyo ya

Kijamii, umekuwa sawa na kauli zinazotolewa na wapinzani wasiokuwa na shukurani ya aina yoyote ile hata wakati huu serikali ikiwaruhusu kuwasiliana na kufanya mikutano ya hadhara tofauti na ilivyokuwa wakati wa Serikali ya Awamu ya Tano!

Kwa hiyo basi, kwa jinsi hiyo, niiombe Serikali yetu makini isifanye ajizi kabisa kwa kuiacha mitandao hiyo kujipachika wadhifa wa upinzani dhidi yake.

*Inaendelea uk. 15*









*Inatoka uk. 14*

Kwani mitandao hiyo inapoandika mambo ambayo ni hatari kwa usalama wa nchi yetu kama hayo na mengine ya uongo kama huu wa kumzushia kifo Makamu wa Rais Dk. Mpango na mikingamo kibao dhidi ya Rais Dk. Samia, kamwe hii haikubaliki. Umefika wakati sasa kama alivyosema Waziri Nape, lazima hawa watu wasakwe na washughulikiwe!

Naamini Serikali haitashindwa kuwakamata, ndiyo kuwakamata na siyo kuwatafuta, kwani vinara wa uzushi mitandaoni wanajulikana. Binafsi habari hizi za uzushi zinazomhusu Makamu wa Rais nilianza kuzisoma kwenye mtandao wa Instagram katika akaunti ya jamaa anayejitambulisha kama 'Kigogo'!

Huyu 'Kigogo' hakuanza leo kuzusha taharuki, aliibuka wakati wa awamu ya tano. Aliivuruga sana nchi, sasa anaendelea hata wakati huu wa awamu ya sita. Hivi ni nani huyu jamaa aliyeshindikana?

Mbali ya huyu jamaa, pia kuna mtandao mmoja mkubwa na maarufu hapa nchini ambao umeachia jukwaa (platform) kwa wasomaji wake kujadili huu uvumi wa kipuuzi wa kifo bandia cha Makamu wa Rais!

Kwa kuwa Waziri Nape kishasema vyombo vyote vya dola wana jukumu la kuwabaini na kuwafikisha mbele ya vyombo vya sheria wale wote walioandaa kadhia hii, mimi nasema tayari wana pa kuanzia!

Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliwahi kusema hivi, "Hakuna uhuru usiokuwa na mipaka. Uhuru usiokuwa na mipaka ni sawa na wendawazimu au ukichaa."

Wakati Mwalimu Nyerere akiyasema hayo, Rais mstaafu wa Awamu ya Tatu, Hayati Benjamin Mkapa, aliwahi kuwaambia waandishi wa habari waliokuwa wakiandika mambo bila mpangilio wala ukweli huku wakidai kubanwa kwa haki zao, aliwajibu kwamba; "Haki haiji bila wajibu".

Nami nishindilie msumari wa moto hayo kwa kuiomba Serikali isipuuze lugha mbaya za mitandao hiyo isiyotimiza wajibu wake wa kuielimisha jamii au kuipasha jamii ukweli wa mambo kwa kuzingatia zaidi utaifa, umoja na usalama wake.

Nasema hivi kwa sababu kinyume cha hivyo, ipo siku nchi hii itaingia kwenye machafuko makubwa yatakayowafanya wananchi wake kuwa wakimbizi ndani au nje ya nchi yao kama vile Wanyarwanda, Warundi, Wasudani Kusini, Wasomali, Watunisia, Wamisri, Wasyria, Wairaki, Walibya na kadhalika.

Matatizo yote hayo huanzishwa polepole na mitandao hiyo ya kijamii na hasa wakati nchi hizi zinapoelekea kwenye chaguzi mbalimbali za ustawi wao.

Mahasimu hao wa Serikali na Taifa, hapa nazungumzia baadhi ya wanasiasa wa upinzani na wanaharakati uchwara huchukua nafasi hizi za kuibuliwa kwa kila aina ya uvumi ovu, kuwachochea wananchi kuchukia serikali yao kwa sababu zisizokuwa na kichwa wala miguu.

Nathubutu kusema hapa kwamba mitandao hii idhibitiwe kwa nguvu zote kwani sasa imedhihirisha kuna binadamu humu nchini hawana chembe ya adabu wala ustaarabu.

Umefika wakati sasa Serikali isisubiri Mamlaka ya Mawasiliano nchini (TCRA) kufanya hivyo, bali yenyewe ichukue jukumu hilo na kuwaadhibu hao wanaozusha habari za utata ambazo nina hakika kuna siku zitaleta maafa makubwa iwapo hazitadhibitiwa.

Ni ngumu kuifungia au kuiwajibisha ile mitandao ya kimataifa kwa vile haikusajiliwa hapa nchini, lakini inawezekana kuwashughulikia Watanzania wote wanaoitumia vibaya mitandao hiyo.



Jamii

# Familia isijitenge na malezi sahihi ya mtoto

**Na Reubeni Lumbagala**

FAMILIA huundwa na mume, mke, watoto, ndugu kama wajomba, kaka, shangazi, baba mdogo, babu, bibi nk. Watoto ni zao la familia. Watoto ni kiungo muhimu cha familia. Watoto wanapozaliwa, ukuaji wao huanzia katika familia.

Zipo taasisi nyingi ambapo zina mchango katika malezi bora ya watoto, lakini familia ni taasisi yenye nguvu kubwa sana katika kuamua aina ya tabia ya mtoto.

Katika makala haya nitachambua nafasi ya familia katika malezi ya watoto. Familia ni taasisi ya kwanza kabisa katika suala la malezi ya watoto katika jamii. Kama wazazi watatimiza wajibu wao huu muhimu wa malezi, mtoto atakuwa katika malezi bora na kuwa mfano bora wa kuigwa katika jamii.

Wazazi, walezi na ndugu wengine wana wajibu mkubwa wa kutoa malezi bora kwa mtoto. Hata Maandiko Matakatifu ya Biblia yanasema "Mlee Mtoto Katika Njia Impasayo, Naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee" (Mithali 22:6). Mtoto ana imani kubwa kutoka kwa wazazi, walezi na ndugu zake wanaomzunguka.

Katika hatua za malezi, ubongo wa mtoto huwa hauna mambo mengi. Na huu ndio muda mwafaka wa wanafamilia kupandikiza mbegu ya malezi bora kwa watoto kabla mtoto hajakumbana na mambo mengine ya kidunia yanayoweza kupata nafasi katika ubongo wake. Malezi ya familia yana nafasi kubwa katika kujenga mambo mazuri kwa mtoto kama vile:

Mosi, kuwa na heshima na nidhamu nzuri. Kama nilivyotangulia kusema familia ndio msingi wa mambo mazuri kwa mtoto. Suala la heshima na nidhamu linaeleweka vizuri kwa mtoto kama wanafamilia watamfundisha katika hatua za awali za maisha yake. Jamii itakuwa na raia wengi wenye heshima na nidhamu. Waswahili wako sahihi kabisa wanaponasema 'samaki mkunje angali mbichi'.

Mbili, kupenda elimu. Kabla mtoto hajapata msisitizo wa kupenda elimu kutoka kwa mwalimu wake shuleni, msisitizo huo anapaswa kuupata kutoka nyumbani kwenye familia anayotoka. Walimu wanapata kazi ngumu ya kuwaelekeza wanafunzi umuhimu wa elimu kwa sababu mtoto anashindwa kuona umuhimu huo kwa sababu watu wake wa karibu wa familia hawamwelezi umuhimu wa elimu.

Kuna kisa kimoja niliwahi kukisikia ambacho kilimtokea mwalimu mmoja ambaye alijibiwa vibaya na mwanafunzi baada ya mwalimu kumsisitiza mwanafunzi huyo umuhimu wa elimu na kusoma. Baada ya Mwalimu kuongea na mwanafunzi kuhusu umuhimu wa elimu, mwanafunzi alimjibu mwalimu kwa dharau akiusema: "Mwalimu acha kufuatilia maisha yangu, baba mwenyewe haniambii nisome, wewe ni nani mpaka uniambie?"

Je, ingekuaje kama mtoto huyu anapata msisitizo wa kusoma kutoka kwa wazazi au wanafamilia wake? Nadhani asingethubutu kumjibu mwalimu wake maneno hayo.

Familia zikisimama kwenye nafasi zao, basi tutawapunguzia kazi walimu wetu kwa mambo ambayo yalipaswa kuanzia kwenye familia. Mwalimu ni mtu wa kusisitiza kile ambacho wanafamilia wameanza nacho nyumbani, lakini kumfanya mwalimu kuwa msemaji mkuu na wa kwanza ni makosa makubwa sana na somo linakuwa gumu kueleweka kwa mtoto.



Tatu, Kupenda na kuyatii mafundisho ya dini. Ili kujenga jamii yenye raia wanaotii mafundisho ya dini, ni muhimu sana familia ikawapa watoto malezi bora ya dini wakiwa watoto wadogo. Ili viongozi wa dini waeleweke kwa urahisi wawapo makanisani na misikitini (madrasa), mafundisho ya dini hupaswa kuanzia nyumbani.

Mwimbaji mmoja wa nyimbo za Injili aliimba wimbo uitwao " Ibada njema huanzia nyumbani". Mtoto aliyelelewa katika kupenda mafundisho ya dini huwa mtoto mwenye tabia nzuri ambazo wanajamii hufurahishwa nazo.

Nne, Kupenda kufanya na kusaidia kazi za nyumbani. Msingi wa mtoto kupenda kushiriki kazi za nyumbani unajengwa katika familia. Baadhi ya wazazi huwandekeza watoto na kufikia hatua mtoto anakatazwa kufanya kazi ndogondogo kama kufua nguo zake, kutandika kitanda chake, kuosha vyombo. Kazi hizi huachiwa dada wa kazi, huku mtoto akitumia muda huo kuangalia runinga.

Hii ina athari mbaya sana hasa pale mtoto anapofikia umri wa kujitegemea, anajikuta hajui kupika, kufua nk. Taasisi ya familia ina jukumu kubwa la kuhakikisha mtoto analelewa katika mazingira ya kupenda kufanya kazi na kusaidia kazi za nyumbani kwa faida yake mwenyewe hapo baadae.

Tano, Kujiepusha na marafiki wasio na tabia njema. Familia pia ina wajibu wa kuhakikisha inatoa mwelekeo na mwongozo mzuri kwa mtoto kuhusiana na aina za marafiki ambao mtoto wao anapaswa kuwa nao. Marafiki wana ushawishi mkubwa sana katika kumfanya mtoto awe na tabia nzuri au tabia mbaya.

Ni muhimu sana kwa wanafamilia kumwelimisha mtoto wao kuambatana na marafiki ambao wataleta matokeo chanya katika maisha yake. Mfano kuwa na marafiki wanaopenda elimu, wenye nidhamu bora, wenye utii, wanaopenda kusaidia wazazi kazi za nyumbani.

Kwahiyo, wanafamilia wana wajibu mkubwa katika malezi ya mtoto ili kumjenga mtoto kuwa na tabia njema na mwelekeo mzuri wa maisha. Kama watoto watapata malezi bora katika familia zao, basi tutajenga jamii yenye raia wema na wawajibikaji kwa maisha yao, jamii na nchi yao. Uwekezaji wa malezi bora ufanywe katika umri mdogo na uanzie katika familia. Tafakari.

Katika kipindi kingine, nitajadili taasisi nyingine zenye mchango wa malezi bora kwa watoto.

*Reubeni Lumbagala ni Mwalimu kutoka Shule ya Sekondari Mlali iliyopo wilayani Kongwa mkoani Dodoma. Mawasiliano yake ni 0620 800 462.*



Paul Mng'ong'o

KLINIKI YA FIKRA

Simu: 0676055444 Email: mngongopaul@yahoo.com

# Mpango wa maendeleo yako binafsi



JUMAMOSI iliyopita katika toleo maalumu la Uhuru, tulimaliza kuangalia mfululizo wa mambo 13 muhimu ambayo watu walio na busara na nguvu ya akili hawayafanyi kwenye maisha yao.

Kwamba mtu anapoamua kuyaacha mambo hayo ndiyo inakuwa sababu ya mtu huyo kusonga mbele kwa haraka.

Lakini bahati mbaya sana ni kwamba, wenye nguvu ya kuyaachahaya miongoni mwetu ni wachache. Wengi wanashindwa kuyaacha mambo haya na kujikuta wakiendelea kuishi maisha ya chini siku zote.

Kama unavyoona kichwa cha habari hapo, juu leo tunaingia kwenye mada nyingine ambayo ni muhimu pia kuifanyia kazi.

Je, Mpango wa Maendeleo Binafsi (Personal Development Plan) ni nini hasa? Huu ni mwongozo kwa maisha na mafanikio yako ya baadaye.

Maendeleo binafsi ni mchakato wa mtu kujiboresha kibinafsi kupitia tabia na shughuli mbalimbali zenye malengo. Ni harakati ya kukua kibinafsi ili kuongeza ubora wa maisha yako na kufikia ndoto na matarajio yako.

Unapoamua kuunda mpango wa maendeleo binafsi, maana yake unanza kutafakari juu ya aina ya mtu unayetaka kuwa, ujuzi unaoutamani, na mafanikio unayoyataka.

Mtu hawezi kuwa zaidi ya uwezo wa fikra zake. Kwa maana nyingine, mtu unayemwona ni zao la fikra zake. Unapoamua kuchukua udhibiti juu ya fikra zako, unaweza kuongoza maendeleo yako binafsi na kuharakisha kufikia unachotaka.

Kuweka malengo ya maendeleo binafsi, kunafungua ulimwengu wa fursa mpya kwako na kuongeza ubora wa maisha yako.

Kuna tofauti kidogo kati ya maendeleo binafsi (Personal Development) na maboresho binafsi (Self Improvement).

Maendeleo binafsi ni kazi unayofanya kubadilisha mwonekano wako. Ni juhudi unazofanya kuendelea katika kazi yako, mtindo wako wa maisha, mtazamo wako, umbo lako, na uhusiano wako na watu.

Kwa upande wa pili, kujiboresha kibinafsi ni mabadiliko ya ndani kuelekea ubora wa tabia, hadhi, au maarifa kwa jitihada zako mwenyewe. Huu ni mchakato wa maisha wa kudumu wa kutafuta njia za kubadilisha tabia zako ili ufikie uwezo wako mkamilifu.

**MAENEO 7 YA MAENDELEO BINAFSI**

Maendeleo binafsi lazima yazingatie ujuzi binafsi, ukuaji wa kibinafsi, na nguvu binafsi. Mambo haya huunda tabia za kujiboresha kibinafsi wakati ukuaji wa kibinafsi unategemea sana elimu na ujuzi. Kuna maeneo saba makuu ya maendeleo binafsi: -

**UJUZI BINAFSI**

Huu unaweza kuwa ule uliozaliwa nao pamoja na ule uliopatikana kupitia mazoezi makusudi. Mifano ya ujuzi binafsi ni kufanya maamuzi, kufanya kazi kwa ushirikiano, kuwa na utaratibu, na mawasiliano.

**UKUAJI BINAFSI**

Hatua hii inaanza na kuwa na mpango wa ukuaji binafsi. Ni hatua za kuelekea kuwa bora zaidi na kutoka katika eneo lako la faraja.

Binadamu na akili ya binadamu vinabadilika kila wakati. Huwezi kuwa mtu yuleyule uliyekuwa mwaka mmoja uliopita. Hii ni jitihada ya kuwa toleo bora zaidi la wewe leo kuliko ulivyokuwa jana.

**NGUVU BINAFSI**

Ni mamlaka ambayo wengine wanakuamini kuwa nayo katika hali fulani na inachochewa na mawasiliano yako, maarifa, na hali yako kifedha.

Nguvu hii inaweza kuzidishwa na mtandao mpana zaidi wa mawasiliano, kutafuta kujifunza zaidi, na kukua kifedha. Nguvu hii inazidisha idadi ya milango ambayo wengine wataiacha wazi ili wewe uingie.

**MABORESHO BINAFSI**

Kujiboresha binafsi ni kujenga tabia njema na kuwa na mtazamo chanya wa kiakili. Kufikiria kabla ya kuchukua hatua, ni muhimu sana katika kukuza kiwango kikubwa cha kujiboresha binafsi.

Ili kukusaidia kufikiri, weka vipaumbele na kuwa na mtazamo chanya wa kiakili ili kufikia malengo yako."

**UWEZO BINAFSI**

Uwezo binafsi unawezakuwa sawa na nguvu binafsi, isipokuwa uwezo ni nguvu unayoiona ndani yako, badala ya jinsi wengine wanavyokuona.

Kukuza taswira chanya na kukumbatia ubunifu katika maisha yako ya kila siku kunaweza kuharakisha muda wa kufikia uwezo binafsi na malengo yako.

> **Kwa upande wa pili, kujiboresha kibinafsi ni mabadiliko ya ndani kuelekea ubora wa tabia, hadhi, au maarifa kwa jitihada zako mwenyewe. Huu ni mchakato wa maisha wa kudumu wa kutafuta njia za kubadilisha tabia zako ili ufikie uwezo wako mkamilifu.**

**TATHMINI BINAFSI**

Ni muhimu kufahamu maeneo ambayo una vipaji asili pamoja na kuchambua maeneo ambayo unahitaji kujiboresha. Hii inaitwa tathmini binafsi. Hapa unatakiwa kuwa mwaminifu kuhusu hali yako ya sasa, kwa kuwa hiyo pekee ndiyo hatua ya kwanza kuelekea mbele.

**MALENGO BINAFSI**

Ndoto hazina maana bila malengo yaliyo wazi. Kuweka malengo ya muda mfupi na mrefu ni hatua muhimu katika kuyatimiza na kukua kama mtu. Kuwa na mpango ulioweka kunakusaidia kuelewa vyema ni mikakati gani inayohitajika.

Kama ungependa kupata ushauri au usimamizi wa karibu katika kuishi mwongozo huu, (Unaweza kuwa Taasisi Binafsi au ya Serikali, Kikundi cha kijamii, Kanisa, Umoja, NGO, Mtu binafsi n.k) Karibu tuwasiliane

Paul Mng'ong'o
Wework Consult - Your Partner in Growth.



Na Hamisi Kibari

Mtanzania wa kwanza kushinda Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu

# Niko tayari kwa kifo - 11

**Chris anampiga mkewe akimtetea hawara yake hadi anapoteza fahamu na kulazimika kumpeleka hospitali baadaye akiwa bado hajitambui. Anawadanganya ndugu wa mkewe kwamba mwanamke huyo ametoweka akimwacha mwanawe mdogo na kwenda kusikojulikana. Daktari anayemtibu mkewe katika wodi ya wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalumu anamjulisha kwamba mkewe amefariki dunia. Daktari huyo anampa njia itakayosaidia asishitakiwe kwa mauaji kutokana na kipigo alichomshushia. Chris anakubali njia hiyo lakini gharama za kuficha kifo hicho ni kubwa. Chris anayewahadaa ndugu za mkewe kwamba yuko katika harakati za kumtafuta, hatokei katika kikao muhimu cha kujulishana mahala alikofikia katika kumtafuta. Lakini dada yake na kaka wa marehemu wanaamkia kwake asubuhiasubuhi. Nini kitaendelea? Fuatana na mtunzi katika kisa hiki.**

"Hapa ni kwa shemeji yako. Kwa nini unabaki nje?" Alihoji Mwalimu Misango akijongea kwenye mlango mkubwa wa nyumba ya Chris baada ya kumwona Jacob akiwa kasimama nje ya nyumba. Ofisa huyo wa Halmashauri ya Manispaa ya Tabora hakujibu kitu zaidi ya kutabasamu na kumsalimia.

Mwalimu Misango alibisha hodi mlangoni kwa Chris. Kutokana na ukimya, alibisha tena mara tatu. Akasikia nyato zinakuja kufungua mlango. Mara mlango ukafunguliwa na Chris ambaye alikuwa amevaa kaptula ndefu ya kulalia na fulana. Akabaki kwa sekunde kadhaa pale mlangoni akitazamana uso kwa uso na dada yake. Chris akakunja uso.

Mtu mwingine akaja nyuma ya Chris kuchungulia akiwa amevaa gauni la kulalia. Alikuwa Joyce. Mwalimu Misango akakunja uso macho yao yalipokutana.

Baada ya salamu, Mwalimu Misango hakusubiri kukaribishwa. Akaingia ndani na Jacob akamtoka nyuma.

"Chris, kwa nini unanizimia simu?" Alihoji Mwalimu Misango kabla hajaketi. Chris ambaye alikuwa akimtoka nyuma na kisha kusimama katikati ya sebule hakujibu kitu. Mama Kessy alirudia swali lilelile. Joyce yeye alipitiliza kwenda chumbani. Mwalimu Misango akamkata jicho la hasira.

"Dada, tuseme umekuja kufanya nini? Wewe si uliniambia mmekwenda polisi. Unajua jana nimefikiria sana. Kwa nini niende kuzungumza na watu wanaokwenda polisi wakati mimi bado ninahangaika kumsaka mke wangu. Yaani wao wana uchungu mkubwa na mke wangu kuliko mimi hata kama kumetokea hali ya kukwaruzana?" Alisema Chris.

"Baba Kenny, kwani kuna shida gani kutoa taarifa polisi kama mtu hajulikani alipo... Siku ya ngapi leo? Hata polisi tuliwaambia tunatoa taarifa kwa niaba yako."

"Pengine si tatizo, lakini mlikua na haraka gani wakati mimi ninaendelea kumtafuta? Kwa nini mwende peke yenu halafu mimi ambaye ndiye mume wake mnipe taarufa tu kama mtu baki. Unajua jana pamoja na kuahidi kuja kwenye kikao nimefikiria sana. Mpaka ninapata hisia kwamba au wewe na ndugu zake ndio mmemficha mama watoto wangu."

"Yaani sisi tumfiche! Tumfiche ili iweje. Yaani unaongea mambo ambayo hayaingii akilini. Au umeamka nazo kichwani?" Aliuliza akimaanisha kwamba pengine alikuwa na ulevi kichwani.

"Sijui nitumie lugha gani ili unielewe… Yaani?""Sikiliza mdogo wangu. Nimekuja tuliongelee suala hilohilo, tena hii ni kwa faida yako. Hebu kaa chini utuambie umefikia wapi. Yaani unashangaza kutulaumu badala ya kuttushukuru kwamba tumekusaidia kutoa taarifa polisi," alisema Mwalimu Misango.

"Dada, mimi ninamtafuta mama watoto wangu na wala sihitaji msaada wenu. Hata kama kumetokea kutoelewana baina yetu lakini ni mama wa wanangu... Kwa sasa sina muda wa kuongea na wewe wala huyu shemeji wakati ninamtafuta Mama Kenny na ninaomba mtulie wakati ninaendelea kumtafuta. Halafu dada mbona mimi sikufuatifuati kwako na kuchunguza maisha yako lakini wewe kila mara unanifuatafuata? Chunga ustaarabu wako na mimi niache na utawala wangu binafsi," alisema Chris kwa hasira.

"Sikiliza Chriss..." alisema Mwalimu Misango.

"Sina cha kusikiliza," alijibu Chris akimkata kauli dada yake. Mtu aliyemsomesha, kumleta mjini na kumsaidia sana kuanza Maisha. Chris aliondoka kuelekea chumbani ambako Joyce alikuwa amesimama mlangoni akiangalia kilichokuwa kinaendelea. Wakaingia ndani na kuwaacha Mwalimu Misango na Jacob wakiwa ameduwaa pale sebuleni.

"Umemkomesha. Simpendi mwanamke huyu. Yaani asubuhi asubuhi majumbani mwa watu? Au anataka umuoe yeye?" Alihoji Joyce wakiwa ndani huku Chris akiendelea kusonya.

"Hivi ninafanya sahihi kweli au ninajipakia makaa? Au ninatakiwa kuwa mpole. Ikija kugundulika kwamba numemuua mke wangu nani atakuwa upande wangu?" Alijiuliza Chris akiwa ameketi kitandani wakati Joye akimpasa mgongoni baada ya kumwona akiwa katika lindi zito la mawazo.

**Dada, tuseme umekuja kufanya nini? Wewe si uliniambia mmekwenda polisi. Unajua jana nimefikiria sana. Kwa nini niende kuzungumza na watu wanaokwenda polisi wakati mimi bado ninahangaika kumsaka mke wangu. Yaani wao wana uchungu mkubwa na mke wangu kuliko mimi hata kama kumetokea hali ya kukwaruzana?**

Sasa Chris alihisi kwamba pengine hatendi adabu kwa dada yake kama mambo yatageuka.

"Lakini mambo yatageukaje wakati Mama Kenny tayari keshazikwa na halmashauri kama mtu asiyejulikana na hakuna mtu anaweza kupata habari zake za pale hospitali?" Alijisema na kujipa nguvu.

Pale sebuleni, Mwalimu Misango akiwa ameduwaa alitamani kwenda kumgongea mdogo wake kwa hasira lakini akasita.

Kama kuna kitu alikuwa anakishangaa, ni mdogo wake kuendelea kumleta hawara kwenye nyumba yenye mkewe wa ndoa. Hii ilikuwa inaleta picha mbaya pia hata kwa macho ya mtu kama Jacob kwamba pengine hajali hata kupatikana kwake.

"Jacob, yaani mapenzi ni kitu kibaya sana. Huyu katekwa na penzi la huyo changudoa hata hajitambui."

"Hata mimi ninaona. Sina hakika kama anamtafuta mkewe. Mimi ningeweza kumwelewa japo kidogo sana kipindi kile dada alipoondoka bila kuaga. Lakini mtu kapotea, kwa maana kwamba, kama kuna sehemu kajificha anaweza kuja muda wowote. Unawezaje kuleta mwanamke mwingine, tena hawara tu, chumbani kwa mkeo? Mwalimu, kuanzia sasa ninaamua kumtafuta mwenyewe mdogo wangu. Ninajua nitampata tu, akiwa hai au mfu," alisema Jacob na kushauri wasipoteze muda kuendelea kuwa pale.

***

Jacob na baba yake mdogo walikaribishwa kuketi katika chumba cha upelelezi katika kituo kikuu cha polisi mkoani Tabora.

Hii ilikuwa ni mara ya pili wawili hao kuja kuonana na askari anayepeleleza tukio la kupotea kwa Tausi, maarufu Mama Kenny kama keshapata habari zozote.

"Mr Chitawo, kama nilivyosema awali, cha msingi mtusaidie sisi polisi katika kumsaka huyu ndugu yenu," alisema askari huyo baada ya Jackson kutaka kujua mahala polisi walipofikia.

"Tunajitahidi sana… Lakini huyu mumewe kwa nini hakamatwi?"

"Tumkamate kwa kosa gani? Yeye tulimwita hapa akatoa maelezo yake. Yeye pia anamtafuta kwa bidii hata dakika 10 zilizopita kanipigia simu akiuliza kama nimesikia lolote... Sasa mnataka tufanye nini?"

"Yeye mlitakiwa kumbana zaidi… Ndiye hasa sababu ya haya yote," alisema Jacob.

"Mr. Chitawo… Hatuendi namna hiyo. Kama nilivyowambia ninawasiliana naye anaendelea kumsaka mkewe. Narudia tena, tushirikiane sote kumsaka nduguyo," alijibu askari mpelelezi.

Jacob alionekana kutoridhishwa na majibu ya askari. Akamgeukia tena yule askari.

"Hebu nikuulize swali bwana askari. Wewe mkeo akipotea katika mazingira unaweza kumltea hawara chumbani kwake? Kwa nini isionekane kwamba huyu mtu anajua mahala mkewe alipo?" "Hiyo, Mr Chitawo ni kesi nyingine," alijibu yule askari. Jacob akahisi bado hajaelewa anachokizungumza.

***

Chris na Joyce walitazama nyumba iliyoko Tambuka Reli, mjini Tabora ambayo walipanga kuhamia. Huku wakiwa pamoja na dalali, mwenye nyumba alianza kupita akiwaonesha vyumba ambavyo viko wazi. Kisha akawaonesha vyoo, bafu na jiko.

Kwa kuwa hawakuwa na familia, kwa maana kwamba Chris alikuwa ametelekeza watoto wake kwa dada yake, alipanga kupanga hata chumba kimoja na sebule au vyjmba viwili. Alipangfa chumba kingine kiwe kama stoo ambambo angehamishiwa vitu vyake vya sebuleni kama makochi na vya jikoni.

"Kodi mtakayolipa, nitarekebisha hicho choo cha chumbani kwenu ambacho kilikuwa hakitumiki pamoja na kupaka rangi," akasema baba huyo mwenye nyumba.

"Kwa sasa kuna wapangaji wangapi hapa?" Alihoji Chris.

"Kuna wapangaji watatu tu. Wawili wamepanga mabanda ya nyuma na mmoja ndo anaishi ndani (kwenye nyumba kubwa)," akajibu baba huyo mfupi na mwenye upara.

"Ee...sasa tunaweza kukaa wapi ili tuandikiane mka…"

Kabla hajamaliza, Joyce alimkatisha: "Samahani kidogo, naomba tuongee faragha kwanza kabla hamjafikia kuweka mikataba."

Joyce hakusubiri jibu la baba mwenye nyumba bali alimvuta pembeni Chris, wakasogea pembeni. Akaongea naye kwa sauti ya chini: "Hii nyumba gani? Mimi siwezi kuishi humu. Nyumba ina wapangaji kibao. Maana yake ni kwamba hivyo vingine viwili navyo vinasubiri wapngaji halafu nyjmba yenyewe ya kizamani sana. Angalia rangi ilivyo hata akipaka rangi mpya nyumba haiwezi kupendeza. Tutaishije humu?"

## VITA VYA ISRAEL, HAMAS:
# 'Mateka walipewa dawa za kulevya'

**YERUSALEM, Israel**

RAIA wa Israel ambao walitekwa nyara na Hamas na kupelekwa Gaza, walipewa dawa za kulevya ili kuwafanya wawe watulivu na wengine kunyanyaswa kingono, kulingana na daktari anayewatibu baadhi ya wale ambao wameachiwa.

Renana Eitan, Mkurugenzi wa Kitengo cha Magonjwa ya Akili katika Kituo cha Matibabu cha Tel Aviv, Sourasky-Ichilov, alisema unyanyasaji wa kimwili, kingono, kiakili na kisaikolojia wa mateka hao walioachiwa huru, ni mbaya sana.

"Sijawahi kuona kitu kama hicho" katika miaka 20 ya kuwahudumia waathiriwa wa kiwewe, alisema. "

Mmoja wa wasichana alipewa ketamine kwa wiki chache," aliongeza. "

Watoto walitenganishwa na familia zao na mgonjwa mmoja alimwambia Eitan kwamba mateka kadhaa walikuwa wamezuiliwa kwenye giza kwa zaidi ya siku nne.

"Walikuwa na akili, walikuwa na ndoto," Eitan aliongeza.

***BBC.***

# 'Israel haitakaa kwa muda mrefu Gaza'



**YERUSALEM, Israel**

WAZIRI wa Ulinzi wa Israel, Yoav Gallant, amesema nchi yake haina nia ya kukaa muda mrefu katika Ukanda wa Gaza.

Gallant amesema wako tayari kufanya mazungumzo kuhusu nani atadhibiti Gaza ili mradi siyo kundi linalochukuliwa hasimu na Israel.

Gallant pia alisema mamia ya wanamgambo wa Hamas mjini Gaza, wamejisalimisha au wamekamatwa katika siku za hivi karibuni, ikiwa ni pamoja na watu walioshiriki katika mashambulizi ya Oktoba 7, mwaka huu.

"Tumezingira ngome za mwisho za Hamas katika miji ya Jabaliya na Shejaiya, katika vita ambavyo vilionekana kuwa haviwezi kushindwa, ambavyo vilitayarishwa kwa miaka mingi kupigana nasi, vinaelekea kusambaratishwa," Gazeti la Times la Israel lilimnukuu akisema.

"Wale ambao watajisalimisha watashughulikiwa kivyao na wale ambao hawatasalimu amri, pia watashughulikiwa kwa njia nyingine," aliongeza.

***BBC.***

# Rais wa Iran kukamatwa

**TEHRAN, Iran**

MALALAMIKO ya kisheria juzi yaliitaka Mamlaka ya Uswizi kumkamata Rais wa Iran wakati wa ziara iliyotarajiwa na kumfungulia mashitaka ya uhalifu dhidi ya ubinadamu uliohusishwa na kukamatwa kwa wapinzani mwaka 1988.

Malalamiko hayo yanamtaka Mwendesha Mashitaka wa serikali ya Uswizi, Andreas Muller, kuhakikisha anakamatwa na kushtakiwa Rais wa Iran, Ebrahim Raisi, kuhusiana na ushiriki wake katika vitendo vya mauaji ya kimbari, mateso, mauaji ya kiholela na uhalifu mwingine dhidi ya ubinadamu.

Raisi alitarajiwa kushiriki katika Kongamano la Kimataifa la Wakimbizi la Umoja wa Mataifa linaloanza leo mjini Geneva, lakini Umoja wa Mataifa ulisema Jumatatu jioni kwamba Waziri wa Mambo ya Nje, Hossein Amirabdollahian, ataongoza ujumbe wa Iran, ishara ambayo Raisi huenda asiwepo.

Malalamiko ya kisheria dhidi yake, yaliyoonekana na Shirika la Habari la AFP, yalichapishwa Jumatatu. Ofisi ya Mwendesha Mashitaka haikuthibitisha mara moja kwamba ilipokea. Yaliwasilishwa na watu watatu wanaodaiwa kuwa waathirika wa ukandamizaji wa Iran dhidi ya wapinzani katika miaka ya 1980.

***VOA***

# Wanajeshi watatu matatani kwa unyanyasaji wa kingono



**TOKYO, Japan**

MAHAKAMA ya Japan imewatia hatiani wanajeshi watatu wa zamani ya kumnyanyasa kingono mwenzao wa kike.

Uamuzi huo wa kihistoria unakuja baada ya Rina Gonoi, 24, kusababisha kilio cha umma na kuvutia hisia za kimataifa alipoweka hadithi yake kwenye YouTube mwaka jana.

Waendesha mashtaka wa Fukushima, waliwafungulia mashitaka watu hao watatu Machi, mwaka huu na kubadili uamuzi wao wa awali.

Japan ni jamii ya kihafidhina ambapo kuzungumzia unyanyasaji wa kingono, bado ni mwiko.

Shutaro Shibuya, Akito Sekine na Yusuke Kimezawa, walipokea hukumu iliyosimamishwa ya miaka miwili katika Mahakama ya Fukushima jana.

Hii ni hukumu ya kwanza kuu dhidi ya unyanyasaji wa kijinsia nchini Japan tangu Juni, mwaka huu wakati nchi hiyo iliporekebisha sheria zake za uhalifu wa kijinsia ambayo ni pamoja na kufafanua upya ubakaji na kuongeza umri wa idhini.

Ilikuwa ni matokeo ya uharakati wa miaka mingi kufuatia msururu wa maamuzi ya mahakama yenye utata ambayo yaliwaachilia watuhumiwa wa shambulizi.

Wanaharakati wanasema sheria za awali mara nyingi ziliwazuia walionusurika kuzungumza.

# Baraza Kuu UN kupiga kura ya kusitisha vita



**NEW YORK, Marekani**

BARAZA Kuu la Umoja wa Mataifa (UN), jana lilitazamiwa kupiga kura kuhusu usitishaji vita mara moja huko Gaza, siku chache baada ya Marekani kupinga azimio kama hilo lililopendekezwa katika Baraza la Usalama.

Rasimu ya sasa iliyopendekezwa ilitolewa na kundi la nchi 20 za Kiarabu na Jumuiya ya Ushirikiano wa Kiislamu.

Hakuna nchi iliyo na kura ya turufu katika Mkutano Mkuu wa wanachama 193.

Walakini, tofauti na Baraza la Usalama, maazimio ya Mkutano Mkuu siyo lazima kisheria, ingawa yanaonesha maoni ya ulimwengu.

Tangu vita kuanza, Baraza la Usalama limeshindwa mara sita kupitisha azimio la kutaka kusitishwa kwa mapigano kwa sababu ya kutoelewana kati ya wanachama wake 15.

# Waasi Houth: Tunahusika shambulio la meli ya mafuta

**ADEN, Yemen**

WAASI wa Kihouthi wanaoungwa mkono na Iran, wamedai kuhusika na shambulizi dhidi ya meli ya mafuta ya Norway.

Kundi hilo lilishambulia meli hiyo kwa roketi baada ya wafanyakazi kukataa kujibu onyo, Reuters imeripoti ikimnukuu Msemaji wa Jeshi la Houthi, Yehia Sareea.

Pia alidai meli hiyo ilikuwa ikibeba mafuta kuelekea Israel, kwa mujibu wa GLZ Radio na kusema Wahouthi walizuia njia meli kadhaa katika siku za hivi karibuni.

Kundi hilo lilisema kwamba wiki iliyopita litashambulia meli zote zinazoelekea Kaskazini mwa Israel.

Pia imezionya kampuni za kimataifa za meli dhidi ya kushughulika na bandari za Israel.

Wafanyakazi wote 22 waliokuwa kwenye meli ya Strinda hawajajeruhiwa, mmiliki wake, Mowinckel Chemical Tankers aliiambia Reuters.

Meli hiyo sasa inaelekea bandari salama, kampuni hiyo ilisema.

***BBC.***

# Thank You Kapteni John Bocco

## ■ Nahodha wa Kihistoria Azam FC, Simba SC

**Na Ibrahim Mkamba**




WAKATI tunaadhimisha miaka 61 ya Uhuru wa Taifa la Tanzania, Taarifa zinasema klabu ya Simba imeamua kumpa mkono wa kwaheri nahodha wa timu yake ya soka, John Raphael Bocco. Pamoja na Simba kumpa mkono wa kwaheri bado inamtaka aendelee kusalia klabuni hapo katika Masuala ya Utawala.

Nia hiyo ni nzuri lakini utekelezaji wake wa kudumu si wa uhakika.

Bocco, aliyeweka rekodi ya kuwa nahodha wa kipekee, akimaliza kuitumikia Simba, ni vizuri asijishushe kurudi Azam FC au kwenda Yanga kukaa benchi.

Wala asiende Ihefu, Kagera Sugar au Geita Gold atakakopata namba. Huko ni kujishusha sana.

Kwanini? Ni kujishusha kwa sababu yeye amekuwa nahodha wa kipekee ndani ya Azam FC kwa misimu yote aliyoitumikia akibeba makombe kuanzia ngao ya jamii, ligi kuu, Mapinduzi, Shirikisho na Kombe la Kagame la Klabu Bingwa Afrika Mashariki na ya kati.

Akawa nahodha Simba kwa kipindi chote alichoitumikia akibeba makombe yote yaliyotajwa isipokuwa Kagame.

Ni nahodha aliyeingia na Simba robo fainali zote za mashindano ya Afrika. Pia amezifunga timu zote kubwa za Simba, Yanga na Azam FC.

Kubwa kuliko yote anaongoza kwa kuwa mfungaji bora wa nyakati zote ligi kuu Tanzania Bara akifunga magoli zaidi ya 200 kwenye viwanja mbalimbali nchini kama si vyote vilivyochezewa mechi za ligi kuu zilizomhusisha.

Mchezaji wa sifa hizi (player of this calibre) hatakiwi kuvuruga sifa hizo kwa kujidhalilisha kwa ilivyoelezwa.

Atangaze kustaafu na astaafu sasa akiwa bado anakubalika.

Simba na Azam FC, zifanye mpango wa pamoja wa kumuaga kwa heshima mchezaji huyo aliyewafanyia makubwa akiwa kiongozi wa wachezaji.

Nia ya Simba ni nzuri lakini uhakika wa kudumu kwa mpango huo haupo.

Hii ni kutokana na uzoefu wa huko nyuma. Wachezaji wengi walifanyiwa hivyo kama njia ya kuwaondoa uwanjani lakini hawakudumu kwenye utaratibu huo. Mfano ni wa Nico Nyagawa na wengine kadhaa. Nia inaweza kujengwa mpango huo uwe wa kudumu lakini viongozi wa taasisi za kiafrika wakibadilika, hutosa watendaji waliowakuta na fagio hilo ni wazi litampitia Bocco na kujikuta yuko mtaani akiwa jobless!

Nini kifanyike? Simba na Azam FC wapange jinsi ya kumpa heshima nahodha wao huyu wa kipekee kwakufanya yafuatayo:-

1. Kuandaa zawadi kubwa zenye hadhi za kumkabidhi kama plot ya ujenzi na vifaa vya ujenzi.

2. Atengenezewe ajira ya uchambuzi wa soka Azam Tv ambapo hata kama mshahara atakaoupata utakuwa mdogo kuliko wa uchezaji, atakuwa na uhakika wa kudumu wa kipato na atakuwa anaendelea kujihusisha na soka, mchezo uliompa heshima kubwa naye kuupa heshima kubwa. Pensheni huwa haizidi wala kufikia ukubwa wa mshahara.

Nimechagua kuchambua soka badala ya ukocha kwa sababu kwanza ukocha lazima mtu awe na matashi nao. Pili, awe na uwezo wa kazi hiyo na tatu ni kazi yenye presha kubwa ambayo haifai kwa mchezaji anayestahili kuendelea kuheshimiwa. Kazi hiyo inaweza kufuta heshima aliyoijenga akiwa mchezaji.

Uchambuzi wa jambo kama soka, sanaa, siasa, uchumi hauhitaji kipaji wala elimu ya kipekee bali ujuzi wa lugha ya kutumika kwa uchambuzi huo na ubobevu kwenye linalochambuliwa kama wa muziki, soka, maigizo, siasa, uchumi, mahusiano ya kimataifa nk. Ikiwa watu ambao hawakucheza soka ya juu ya ushindani leo ni wachambuzi wa kuheshimika wa soka, Bocco atashindwa nini na uzoefu wake wote wa ushirikiano na mawasiliano uwanjani, tabia tofauti za makocha tofauti kwenye viwanja vya mazoezi na ndani ya vyumba vya kubadilishia nguo, tabia tofauti za waamuzi wa soka na mifumo mbalimbali ya uchezaji na jinsi ya kuibadilisha uwanjani kwa jinsi wapinzani wachezavyo nk. Akipata fursa hiyo, Bocco atatoa mchango mkubwa wa elimu ya soka ya kuchezwa.




3. Zawadi zote hizo na nyingine akabidhiwe kwa kuzitangaza siku ya mechi maalum ya kumuaga ya Simba na Azam FC.

4. Utaratibu wa mechi hiyo uwe kipindi cha kwanza achezee Azam akiwa nahodha na kipindi cha pili achezee Simba akiwa nahodha.

5. Kwa pande zote mbili, wachezaji wacheze kwa kubadilishana ili wengi aliocheza nao akiwa Azam kama Frank Domayo, Salum Abubakar, Mudathir Yahya, Himid Mao, Kipre Tcheche na wengine wote watakaopatikana wacheze naye na baadhi dhidi yake. Na kwa Simba hivyo hivyo kwa akina Miraji Athuman Madenge, Francis Kahata, Rally Bwalya, Thadeo Lwanga, Meddie Kagere, Chris Mugalu, Laudit Mavugo, Shiza Kichuya Emmanuel Okwi na wengine watakaopate nafasi ya kucheza naye kumuaga kwa watakaopatikana.

6. Wale aliochezanao Azam na Simba wasiokuwepo kokote kwa sasa kati ya timu hizo kama kina Gadiel Michael, Pascal Wawa , Erasto Nyoni na wengine wacheze kwa Azam na hii itatokana na uboreshaji wa mpango huo. Itapendeza kama mechi hiyo itahusisha zaidi wachezaji aliocheza nao kwenye timu hizo na si kina Feisal au Kipre Junior ambao ili squad ienee itabidi wengi wao wacheze pia. Kipindi atakachochezea Simba, nahodha wa Azam FC awe Morris.

# Walinda mlango bora katika soka la Africa



**Na Valensi Mbaga**

WAKATI wowote kunapokuwa na majadiliano kuhusu makipa bora zaidi duniani, mikono salama ya Italia, Gianluigi Buffon, Peter Cech, na majina kadhaa huibuka Majina kadhaa kutoka Afrika yanakuja, pia; kama Thomas N'Kono, Joseph-Antoine Bell, Mnigeria Vincent Enyeama, na baadhi ya wengine wanatajwa kwa heshima.

Hii hapa orodha yetu ya makipa bora wa Afrika duniani kwa sasa.

**5. Dennis Onyango**

Onyango ambae anakipiga katika klabu ya Mamelodi Sundowns ni kipa mkongwe ambaye hajafanya vema nje ya ufukwe wa Afrika lakini bado anachukuliwa kuwa kipa mkubwa.

Licha ya kuwa na umri wa miaka 37, Onyango bado anafanya vizuri katika ligi ya Afrika Kusini na bado anaendelea kuonyesha ubora mkubwa katika Ligi ya Mabingwa ya CAF.

Alicheza mechi 82 akiwa na Uganda na kuwa nahodha hadi alipostaafu kimataifa mnamo 2021.

Dennis Onyango anajulikana kwa uwezo wake wa kuokoa penalti na ubora wa kuokoa mpira katika mashambulizi ya kushtukiza na akiwa na mshambuliaji mmoja.

**4. Mohammed El Shenawy**

El Shenawy, mwenye umri wa miaka 34, anaweza kuwa anaelekea mwisho wa maisha yake ya soka, lakini labda anaelekea kwenye mpambano mwingine wa kuvutia katika s afari yake ya soka.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Misri na klabu ya Al Ahly anaweza asivutie kutoka nje ya nchi, lakini labda anaweza kuvutia macho yao wakati Michuano ya Mataifa ya Afrika itakayofanyika mnamo Januari 2024.

**3. Andre Onana**

Mcameroon André Onana amezua mzozo katika miezi michache iliyopita, kutokana na kiwango anachokionyesha kwa waajiri wake wapya Manchester United. Walakini, Onana ni mmoja wa makipa bora wa Kiafrika katika kizazi chake.

Kiwango bora na cha kuvutia huko Inter Millan kilimwezesha kuhamia United , na kwa sasa André Onana ndiye golikipa bora wa Kiafrika barani Ulaya.

**2. Yassine Bounou**

Kwa upande wa uchezaji, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 ndiye kipa bora zaidi barani Afrika sio tu kwa nambari zake za Kombe la Dunia la 2022 lakini pia kwa sababu ya kucheza kwake katika kiwango cha vilabu.

Bounou alienda kwenye Kombe la Dunia nchini Qatar na kwenda nusu fainali bila kufungwa na mchezaji wa upinzani.

Ni Bao lake pekee lilikuwa la kujifunga katika mchezo wa tatu wa hatua ya makundi dhidi ya Canada.

Kwa jumla, aliruhusu mabao 3 katika mechi saba za kombe la dunia, huku mawili kati ya hayo yakifungwa 2-1 na Croatia katika mechi ya mshindi wa tatu.

Yassine pia ni mmoja wa makipa bora zaidi kwenye Ligi ya Saudia anapoitumikia timu ya Al Hilal na anasifika kwa uchezaji wake wa uhakika katika goli na akili timamu.

Na kwa sasa ndie mshindi wa tuo ya Golkipa bora wa Africa kwa mwaka 2023-24

**1. Edouard Mendy**

Kipa wa Senegal ni nambari moja barani Afrika kulingana na wasifu wake kabla ya 2022, akiwa sehemu ya mafanikio ya 2021 kwa Chelsea.

Tuzo zake Binafsi ni pamoja na Kikosi Bora cha Ligi ya Mabingwa ya UEFA: 2020–2021, Kipa Bora wa Msimu wa UEFA Champions League: 2020–2021, Kipa Bora wa Wanaume wa FIFA: 2021, Kipa Bora wa Kombe la Mataifa ya Afrika: 2021, na Kombe la Afrika la 2021, Timu ya Mataifa ya Mashindano: 2021.

Alianza mwaka wa 2022 kama mshindi wa AFCON akiwa na Senegal, lakini uchezaji wake umekuwa ukitofautiana kwa klabu na nchi.

Vivyo hivyo kwenye Kombe la Dunia huko Qatar, ambapo aliruhusu mabao saba katika mechi nne.

Kabla ya Mundial, alipoteza jezi yake namba moja kwa Kepa Arrizabalaga akiwa Chelsea, na baadae kutimkia Saudi Arabia ambapo anawatumikia matajiri wa Al Ahli.

Pamoja na yote, kizazi kipya cha makipa kinazidi kung'ara barani Ulaya, na makipa kadhaa wa Kiafrika ni sehemu yao.Wachezaji wengi wa Afrika wameng'ara katika ligi kuu zote za










Onyango ambae anakipiga katika klabu ya Mamelodi

# Buriani Mtunzi wa "LOLIWE" Zahara

Na Muhidin Issa Michuzi

JUMAPILI ya Desemba 15, 2013, Rais wa kwanza Mwafrika wa Afrika Kusini, Mzee Nelson Mandela alizikwa kijijini Qunu katika mazishi ya Kitaifa yaliyoshuhudiwa dunia nzima. Alizikwa kwa heshima zote za kiongozi wa Taifa na Chifu wa kimila katika sehemu aliyochagua mwenyewe kuwa nyumba yake ya milele.

Nashukuru nilikuwa miongoni mwa waliohudhuria mazishi hayo ya karne yaliyosheheni watu mashuhuri toka kila pembe ya dunia. Pichani nikiwa hapo mazishini na mcheza sinema wa Uingereza Idris Elba ambaye alicheza kama Mandela kwenye filamu ya "Long Walk to Freedom"

Ni siku ambayo inanikumbusha sana wimbo "Loliwe" (Treni) wa Msanii wa Afrika Kusini Bulelwa Mkutukana aliyejulikana kama Zahara kwani wakati huo ndio ulikuwa umetoka na uko katika chati za juu ulimwenguni kote. Na Mashairi yake yaliendana vyema na huo msiba ulioikumba dunia wakati huo.

Mie na mwenzangu Adam, tukisafiri kwa gari kwa zaidi ya saa saba toka Pretoria, tulikuwa tunapiga CD ya nyimbo za Zahara njia nzima. Na Dereva wetu Maphumo alitutafsiria neno kwa neno. Tukawa tunauimba njia nzima. Hadi leo naujua kwa moyo, maana si mrefu kihivyo, sema una Mashairi ya kujirudia rudia.

Albamu ya "Loliwe" ilishinda tuzo kibao, ikiwemo Albamu Bora kwa kuuza, Albamu ya Mwaka na Albamu Bora ya Muziki ya Urban, katika Tuzo za Kila Mwaka za 18 za Muziki za Afrika Kusini, illiteuliwa kuwa Albamu Bora iliyozalishwa nchini humo na pia ikashinda Albamu Bora ya Kike katika Tuzo za Muziki za Metro FM za Mwaka 2011.

Usiku wa kuamkia leo sikuamini niliposikia Zahara katutoka. Na wazo la kwanza kunijia ni hiyo safari ya mwenda Qunu kwenye mazishi ya Madiba. Pumzika kwa Amani Zahara.

uLoliwe wayidudula, uLoliwe wayidudula (treni linasukuma, treni linasukuma)

> "Albamu ya "Loliwe" ilishinda tuzo kibao, ikiwemo Albamu Bora kwa kuuza, Albamu ya Mwaka na Albamu Bora ya Muziki ya Urban, katika Tuzo za Kila Mwaka za 18 za Muziki za Afrika Kusini, iIliteuliwa kuwa Albamu Bora iliyozalishwa nchini humo na pia ikashinda.



uLoliwe wayidudula , Nang'esiza (treni linasukuma, hilo linakuja)

uLoliwe wayidudula, uLoliwe wayidudula (treni linasukuma, treni linasukuma)

uLoliwe wayidudula , Nang'esiza (treni linasukuma, hilo linakuja)

Sul'ezonyembezi mntakwethu, Sul'ezonyembezi mntakwethu (futa Hayo machozi, kipenzi)

Sul'ezonyembezi mntakwethu. Nang'esiza (futa hayo machozi kipenzi, hilo linakuja)Sul'ezonyembezi mntakwethu, Sul'ezonyembezi mntakwethu (futa Hayo machozi kipenzi)Sul'ezonyembezi mntakwethu. Nang'esiza (futa Hayo machozi kipenzi, hilo linakuja)

(Korasi)

Phezulu, eNkosiniKuhlal 'ingcwele zodwa (mbinguni, kwa Mungu, huishi watakatifu tu)

Mawufuna ukuya khona, thandaza (kama wataka kwenda huko, sali)

Phezulu, eNkosini, Kuhlal 'ingcwele zodwa (mbinguni, kwa Mungu, Huishi watakatifu tu)

Mawufuna ukuya khona, thandaza (kama wataka kwenda huko, sali tu)



Michuzi na Idriss Elba







# Kona ya Urembo

Na Hidaya Machuppa Simu: +255 765 828 219

# Pendeza kwa kuvalia nguo NYEUPE





KWA mitindo, rangi nyeupe hutumiwa kuamsha hisia ya usafi, kutokuwa na hatia, upya au usafi. Kwa sababu nyeupe huakisi mwanga.

Kufikia miaka ya 1950, wanajarida ya wanawake yalianza kufanya sheria hii ya " kutokuwa na uweupe baada ya siku ya wafanyakazi" hadharani zaidi. Kuvaa nguo nyeupe pekee Kati ya siku ya ukumbusho na Siku ya wafanyakazi sasa kuliashiria kuwa mwanamke alikua sehemu ya klabu inayojulikana ya mitindo. Kuvaa nyeupe inaweza kuonekana kuwa ya zamani, lakini kwa kweli bado kuna matukio mengi ambapo gauni nyeupe inaweza kuwa mavazi ya kufaa zaidi. Rangi katika nguo mara nyingi ni ishara, ambayo inamaanisha kuwa unaweza kuelezea wazo fulani au maana kwa kuchagua rangi maalum, na nyeupe sio ubaguzi kwa sheria hii.

Ingawa rangi angavu ni wazi na ya kufurahisha kuongeza kwenye kabati lako la nguo, nyeupe pia ni sehemu muhimu ya mavazi yako rasmi. Hapa kuna hafla tano maalum ambazo zitafaidika kutokana na vazi jeupe la kifahari

Siku ya harusi yako ni jibu dhahiri zaidi wakati utahitaji mavazi nyeupe. Utamaduni wa Magharibi umefuata kwa muda mrefu mila ya kuvaa nyeupe siku ya harusi ya mtu.

Je, ni njia gani bora ya kuanzisha ndoa yako kuliko kwa ishara inayowakilisha mwanzo safi wa sura muhimu katika maisha yako? Urahisi ni mzuri kila wakati, haswa ikiwa unataka mavazi yako ya harusi kuwa muhimu zaidi kuliko mtindo.

**Kuzaliwa na baraka**

Kama vile nyeupe inamaanisha mwanzo mpya wa ndoa, nyeupe pia ni muhimu kwa kuzaliwa na ibada za kidini kwa watoto. Miongoni mwa mambo mengine, madhumuni ya ubatizo na baraka za mtoto ni kumtambulisha mtoto au mtoto katika jumuiya ya marafiki, familia na waabudu wenzake, anasema Huggies.

Chochote kutoka kwa kanisa la ubatizo hadi sherehe rahisi ya kumtaja inaweza kuongezwa na mavazi mazuri nyeupe kwa mtoto, Ikiwa una baraka ya mtoto inayokuja kwa mdogo wako, mavazi nyeupe inaweza kuwa chaguo kamili kwa mavazi yako kwa tukio hilo.

**Ubatizo**

Wakati ubatizo unatokea, maana ya mfano ya kutakaswa na kuzaliwa upya inabakia sawa. Ibada za kidini na mavazi yanayohusiana nayo yamekuwa muhimu kila wakati, na nyeupe mara nyingi ni rangi ya kawaida inayotumiwa kuonyesha kujitolea na usafi wa juu wa kidini. Iwe ni ubatizo wako au ubatizo wa mtoto wako, vazi jeupe litafaa kwa tukio hilo.

**Mikusanyiko ya majira ya joto**

Mbali na rangi nyeupe kuwa na maana ya ndani zaidi katika mavazi na ibada za kidini, ni rangi ya kustarehesha sana kuvaa wakati wa joto la kiangazi, na imekuwa ni lazima kwa kabati la nguo la mwanamke Iwe unahudhuria karamu ya kupendeza ya bustani au unaenda kuonana na mpendwa. rafiki hutumbuiza katika ukumbi wa hali ya juu wa nje, akiwa amevalia mavazi meupe daima huonyesha darasa na uboreshaji.

Kulingana na mtindo unaotaka, unaweza kuchagua kitu rahisi zaidi na cha kawaida, au vazi linaloonyesha upendo wako kwa mavazi mepesi na ya baridi. Zaidi ya hayo, nyeupe inakamilisha tani nyingi za ngozi hivyo itakuwa daima kutoa faida katika hali yoyote ya kijamii.

**Kwenda hekaluni**

Washiriki wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho wanaweza kuhudhuria hekalu ili kupokea taratibu takatifu za kidini wanapofikia utu uzima.

> **"Wakati ubatizo unatokea, maana ya mfano ya kutakaswa na kuzaliwa upya inabakia sawa. Ibada za kidini na mavazi yanayohusiana nayo yamekuwa muhimu kila wakati, na nyeupe mara nyingi ni rangi ya kawaida inayotumiwa.**



Leo yetu ndiyo kesho yetu
Uelekeo Spoti
| Jumatano Desemba 13-19, 2023 |

## Rasmi Taifa Cup Dodoma

**Na Mwandishi Wetu**


MICHUANO ya Kombe la Taifa kwa mpira wa Wavu itafanyika Dodoma mwaka huu.

Mashindano hayo ya mikoa itaanza Desemba 18 hadi 23 mwaka huu katika viwanja vya Chinangali.

Mwenyekiti wa Shirikisho la Mpira wa Wavu Tanzania (TVF), Mhandisi Magoti Mtani alisema wanaendelea na maandalizi ya michuano hiyo.

Kombe la Taifa linafuatia michuano mingine makubwa ya wavu ya Nyerere ambayo ilishirikisha klabu kutoka nchi za Afrika Mashariki na kufanyika mkoani Kilimanjaro.

Mtani alisema dhumuni la kupeleka michuano hiyo Dodoma ni kuhakikisha mchezo unawafikia watu wengi Zaidi.





# Serikali yaishukia Yanga

**Na Mwandishi Wetu**

YAMEWAKUTA Mabingwa watetezi wa soka Tanzania Bara, Yanga ya Dar Es Salaam.

Serikali imeshusha rungu lake kwao kutokana Na kitendo kinachodaiwa kufanya na mashabiki wake kung'oa Viti wakati wa mechi Kati ya Yanga na Al Ahly ya Misri.

Katika pambano hilo la Klabu Bingwa Afrika, mashabiki wa Yanga waliwasha fataki na kusababisha vurugu za ung'oaji Viti.

Taarifa ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, imewataka Yanga kuwasiliana na Uongozi wa Uwanja WA Benjamin Mkapa ili kujua hasara iliyopatikana na kugharamia.

Siku chache baada ya pambano hilo, Naibu Waziri wa hiyo, Hamis Mwinjuma alisema serikali haitalifumbia macho suala hilo na wahusika watasakwa.

Katika taarifa zisizo rasmi Yanga wamekuwa wakikana kuhusika na uharibifu huo na wakiwabebesha mzigo mashabiki wa Simba kuwa ndio wenye tabia hiyo.

## Refa apewa kisago kizito

**ANTWERP, Uturuki**

RAIS wa Klabu ya Ankaragücü, Faruk Koca ameingia uwanjani baada ya Mchezo kumalizika baina ya Ankaragücü na Rizespor akamtwanga ngumi nzito refa wa mchezo huo.




Koca alimtandika mwamuzi Halil Umut ngumi iliyompeleka chini kwakile alichodai refa huyo kutoa maamuzi aliyoyaona hayapo sawa kutokana na kuamuliwa na VAR.

katika mchezo wa ligi Kuu Uturuki 'Super Lig' iliyofanyika Jumatatu usiku kulitokea tukio la aibu uwanja huo wa soka kugeuka kuwa ulingo wa ndondi.

Refa huyo alikubali bao la dakika za mwisho katika sare ya 1-1.

Mwamuzi huyo ambaye alionekana jicho likiwa jeusi baada ya shambulio hilo, alipigwa ngumi na mateke alipokuwa uwanjani katika dimba la Eryaman.





Shirikisho la Soka Nchini Uturuki limeripotiwa kuamua kufanya mkutano usio wa kawaida baada ya tukio hilo la kushangaza.

Rais Koca ameripotiwa kuhitaji matibabu hospitalini lakini waziri wa mambo ya ndani wa Uturuki, Ali Yerlikaya, amesema "taratibu za kutiwa kizuizuni zitatekelezwa baada ya matibabu hayo huku adhabu za haraka ikitarajiwa kufuata.

## Benchikha, Mayele waishia tatu Bora

**Na Mwandishi Wetu**

MSHAMBULIAJI wa klabu ya Napoli na timu ya Taifa ya Nigeria Victor Osimhen ameshinda tuzo ya mchezaji bora wa kiume wa mwaka 2023 akiwapiku Hachraf Hakimi (Morocco) na Mohamed Salah (Misri).

Mshambuliaji wa Barcelona na timu ya Taifa ya Wanawake ya Nigeria, Asisat Osoala ameshinda tuzo ya Mchezaji bora wa Mwaka Afrika kwa Wanawake akiwapiku Thembi Kgatlana wa Afrika Kusini na Barbara Banda wa Zambia.



Golikipa wa Al Hilal ya Saudi Arabia na timu ya Taifa Morocco, Yassine Bounou ameshinda tuzo ya kipa bora wa Mwaka 2023 Afrika akiwabwaga Andre Onana wa Cameroon na Manchester United na Mohamed El Shenawy wa Misri na klabu ya Ah Alhy.

Winga wa Al Ahly ya Misri na Timu ya Taifa ya Afrika Kusini, Percy Muzi Tau ametwaa Tuzo ya mchezaji bora wa Vilabu vya ndani Afrika.

Tau amewashinda Peter Shalulile wa Mamelodi na Fiston Mayele wa Pyramids.

Kocha timu ya Taifa ya Morocco, Walid Regragui ameshinda tuzo ya kocha bora wa mwaka 2023 baada ya kuiongoza Morocco kumaliza nafasi ya nne kwenye michuano ya Kombe la Dunia la Qatar 2022.

Regragui amewashinda kocha wa Simba SC, Abdelhak Benchikha na Aliou Cisse wa Senegal.

Vigogo wa Misri na Mabingwa wa Ligi ya Mabingwa Afrika 2023, Al Ahly wameshinda tuzo ya klabu bora ya mwaka kwa Wanaume Afrika.

Timu ya Wanawake ya Mamelodi Sundowns ambao ndio Washindi wa Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake imeshinda tuzo ya timu Bora ya Mwaka Afrika kwa Wanawake.